# Nipashe

Alhamisi Desemba 31, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580446

www.ippmedia.com

The Guardian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

**MIMEA** vamizi 69 yatikisa katika hifadhi za taifa

UKURASA 3



**RIPOTI MAALUM -2**
Shida kuu kijiji kisicho na zahanati miaka 46

UKURASA 7




UKURASA 11

# Utata wagubika kifo mmiliki banda la chips

UKURASA 2



Yusufu Deus (kushoto), akipatiwa msaada wa fedha kutoka kwa mchungaji wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Usharika wa Kijitonyama jijini Dar es Salaam, Mchungaji Eliona Kimaro, wakati wa uhai wake.

Eneo la biashara ambalo Yusufu alikuwa anafanyia kazi

## Watoto wafa kwa kuungua moto wakiwa wamelala

UKURASA 2

## Wastaafu walia mifuko kuchelewesha mafao yao

UKURASA 3

**MICHEZO** **POLISI TANZANIA, AZAM MCHUANO WA HESHIMA** UK. 23

**MAONI, KATUNI** UK. 6

HABARI KITAIFA



Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhandisi Dk. Leonard Chamuriho (kulia), akitoa maelekezo kwa Meneja wa Wakala wa Barabara Nchini (TANROAD) Mkoa wa Pwani, Mhandisi Wilicis Mwageni, alipokuwa akikagua maendeleo ya mradi wa Kituo cha pamoja cha Ukaguzi (OSBP), mkoani Pwani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Utata wagubika kifo cha mmiliki banda la chipsi

**Na Romana Mallya**

UMETATA umegubika kifo cha mmiliki wa banda la chipsi, Yusufu Deus, baada ya mwili wake kukutwa ukining'inia katika eneo lake la biashara ikiwa ni wiki chache baada ya kutekwa na watu wasiojulikana na kupatikana siku saba baadaye.

Kabla ya umauti, Deus alikuwa anamiliki banda la kukaanga chipsi maeneo ya Kijitonyama wilayani Kinondoni jijini Dar es Salaam.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Kipolisi Kinondoni, Ramadhan Kingai, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo alipotafutwa na Nipashe jana na kwamba uchunguzi wake unaendelea.

Nipashe pia ilimtafuta Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, ambaye hata hivyo alidai hakuwa na taarifa za tukio hilo.

Kwa mujibu wa mke wa marehemu, Neema Erick, tukio hilo la mwili wa mumewe kukutwa ukining'inia kwenye eneo lake la biashara, lilitokea usiku wa kuamkia Jumatatu ya wiki hii.

Neema alidai kuwa Jumapili asubuhi, mume wake alipoamka, alijiandaa na kwenda Kanisa la Kiinjili la Kirutheli Usharika wa Kijitonyama ambako alikuwa mwimbaji wa kwaya ya kanisa hilo.

"Baada ya ibada ya Jumapili, alirudi nyumbani saa tano asubuhi na alilala na ilipofika saa nne usiku, aliniaga anakwenda kununua umeme, lakini cha kushangaza hakurudi tena.

"Baada ya kuhangaika usiku kucha kumtafuta, ilipofika saa nne asubuhi, nilipata taarifa kuwa mwili wake umekutwa ukiwa unaning'inia eneo lake la kazi," alisimulia.

Neema alidai kuwa kabla ya tukio hilo, Desemba 2 mwaka huu, mume wake alitekwa na watu wasiojulikana na walikaa naye kwa muda wa siku saba na kupatikana maeneo ya Kijitonyama, Makumbusho Desemba 8, mwaka huu.

Alisema baada ya tukio hilo la utekaji, mume wake alikaa nyumbani bila kwenda kwenye biashara zake kwa muda wa wiki moja.

Alisema kuwa mume wake amemwacha na watoto wawili na kwamba mazishi yake yanatarajiwa kufanyika mkoani Shinyanga baada ya kukamilika kwa uchunguzi wa mwili wake unaoendelea katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Mchungaji wa Kanisa la KKKT Kijitonyama, Eliona Kimaro, wakati wa ibada kanisani hapo hivi karibuni, aliwaeleza waumini kuwa, alipata taarifa za kutekwa kwa mfanyabiashara huyo na watu wasijulikana ambao walimchukua kazini kwake na kumpeleka porini na kukaa naye kwa siku saba.

Akisimulia mkasa huo, Mchungaji Kimaro alidai kuwa baada ya mfanyabiashara huyo kutekwa, alipatikana siku ya saba akiwa ametupwa eneo la Kijitonyama, mwili wake ukiwa na majeraha.

"Nilifanikiwa kuzungumza na Yusufu, alikuja ofisi kwangu akiwa na maumivu makali, alinieleza kuwa kabla ya tukio hilo, walifika watu watatu (alitaja mwonekano wao) katika eneo lake la biashara wakitaka awaeleze mganga ambaye anayemwezesha kuuza chipsi kwa kiwango kikubwa.

Alisema watu hao walitaka Yusufu awapeleke kwa mganga wake ambaye wanamaani amempa dawa ya kufanya biashara na kuwa na mapato ya zaidi ya Sh. milioni moja kwa siku.

"Lakini, Yusufu aliwaeleza kuwa hana mganga, anasali KKKT Kijitonyama na mchungaji wake ni Kimaro na aliwataka kama wako tayari, awalete hapa, lakini watu hao walitaka mganga aliyempa dawa," alidai.

Mchungaji Kimaro alisimulia kuwa, watu hao hawakuamini na kwamba siku iliyofuata, walirudi tena na kumsisitiza awatajie mganga anayemwezesha kufanya biashara hiyo kwa faida kubwa.

Alisema licha ya Yusufu kuwaeleza ukweli aliyemsaidia ni Mungu watu hao hawakuridhika waliondoka na siku ya tatu yake walifika tena na ndipo wakamteka na kumwingiza kwenye gari aina ya Noah na kuondoka naye.

"Yusufu alinisimulia kuwa, wale watekaji walisafiri naye kwa muda wa siku mbili akiwa amewekwa chini ya siti, aliweza kujua muda kupitia saa yake ya mkononi, alisema watu hao walimnyang'anya fedha Sh. milioni 1.7 na simu yake ya mkononi," alisema.

Alisema wakiwa porini, watu hao walikuwa wakiwasiliana na mtu ambaye ndiye aliyewatuma watekeleze tukio hilo ambaye aliwataka wamuue kijana huyo kisha atawalipa fedha.

"Wakiwa porini, huku wakimpa Yusufu maji na mkate, waliendelea na mawasiliano na mtu aliyewatuma, lakini mtu huyo hakutuma fedha. "Yusufu alianza kuumwa jino na alipowaeleza maumivu anayoyapata, mmoja wa waliomteka alimwonea huruma, akatoka kwenda kutafuta dawa na kurudi na Panadol ambazo alitumia na maumivu kupungua.

"Yusufu alinisimulia kuwa, wakati wote wakiwa porini, wale watu walikuwa wakiwasiliana na mtu aliyewatuma bila mafanikio na ndipo miongoni mwao walipotaka wamuue Yusufu, waondoke, yule alikwenda kununua dawa, alisimama upande wa kijana huyo kumtetea," alidai.

Mchungaji huyo alidai kuwa mmoja wa watekaji hao, aliwaeleza wenzake kuwa kwa sababu wameshapata fedha walizochukua kwa Yusufu, haoni haja ya kumuua.

Alisema baada ya mabishano ya muda mrefu ndipo watu hao walipokubaliana wamrudishe Dar es Salaam na walifanya hivyo na kwenda kumtelekeza eneo la Kijitonyama, Makumbusho jijini.

Juzi, Mchungaji Kimaro aliwatangazia waumini wa kanisa hilo kuwa Yusufu amefariki dunia baada ya mwili wake kukutwa eneo lake la biashara ukiwa unaning'inia.

Keneth John, mmoja wa wafanyakazi kwenye banda hilo la chipsi, alisema jana kuwa alifika katika eneo la biashara saa 12 asubuhi na alipoingia getini ndipo alipoona mwili wa bosi wake ukiwa unaning'inia.

"Mlango wa mbele wa fremu ya biashara ulikuwa umefungwa kama kawaida, nilipitia geti kubwa ambalo lipo nyuma ya fremu na huko kuna nyumba za wapangaji, nilipoingia kuelekea kwenye fremu, ili kufungua kuchukua ndoo ya kwenda kununua nyama, ndipo nikamkuta bosi akiwa ananing'inia.

"Sikuelewa, nilitoka nje na kumwita dada mmoja mfanyabiashara wa saluni, naye alikuja kushuhudia na ndipo taarifa zilifika polisi wakaja kuchukua mwili," alisimulia.

## Wafa kwa kuungua moto wakiwa wamelala

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

WATOTO wawili wamefariki dunia kwa kuungua moto wakiwa wamelala kwenye kibanda walichokuwa wakiishi, huku mwingine akifia njiani akipelekwa hospitalini.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kigoma, Kamishna Msaidizi (ACP) James Manyama, alisema jana kuwa watoto hao walipoteza maisha kwenye matukio mawili tofauti ya ajali ya moto katika wilaya za Uvinza na Kasulu mkoani hapa.

ACP Manyama alisema jana kuwa tukio la kwanza limetokea Desemba 27 majira ya saa 7:00 mchana eneo la Mpanzi, Kijiji cha Nyarugusu wilayani Kasulu.

Alisema katika tukio hilo, watoto Yumwema Festo mwenye umri wa miaka miwili na Enifa Festo (miezi mitatu) wote wa familia moja, waliungua moto na kufariki dunia wakiwa wamelala ndani katika kibanda walichokuwa wakiishi.

Familia hiyo, alisema ni ya watu wanaodaiwa kuwa wahamiaji haramu kutoka Burundi waliokuwa wakifanya kazi mashambani.

Kamanda Manyama alisema baada ya tukio hilo, wazazi wa watoto hao wamekimbia huku Jeshi la Polisi likiendelea kuwatafuta.

Alisema tukio lingine ni la mtoto wa mwaka mmoja, Rose Kessy, aliyepoteza maisha juzi akiwa njiani kupelekwa hospitalini baada ya kuungua moto Desemba 29, mwaka huu.

Manyama alisema katika tukio hilo, mtoto huyo aliungua moto akiwa ameachwa kwenye jiko la mkaa anapika wakati mama yake akiwa amekwenda kisimani kuchota maji.

Alisema uchunguzi wa awali unaonyesha kwamba tukio hilo lilisababishwa na upepo kurusha cheche kwenye nyumba ya nyasi alimokuwa mtoto huyo.

''Bado tunachunguza matukio hayo ili kubaini kama kuna mkono wa binadamu au la," alisema.

Kamanda Manyama alisema miili ya watoto wawili wa familia moja imehifadhiwa katika Kituo cha Afya cha Nyarugusu, huku mwili wa mtoto mwingine ukihifadhiwa katika Kituo cha Afya cha Nguruka kwa uchunguzi zaidi.

# Walia kucheleweshewa mafao wanapostaafu

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WATUMISHI wanaokaribia kustaafu utumishi wa umma na sekta binafsi, wameomba waajiri kuwaandalia mafao yao mapema, ili kama kuna kasoro zitatuliwe mapema.

Pia wameelezea kucheleweshewa mafao yao baada ya kuondoka katika utumishi, hali ambayo inawafanya waishi katika mazingira magumu baada ya kustaafu.

Hayo yalisemwa jana wakati wa mafunzo ya kujiandaa kustaafu utumishi kwa wafanyakazi wa Wizara ya Maliasili na Utalii na taasisi zilizo chini yake yanayofanyika mjini hapa.

Walisema hali hiyo imekuwa ikiwasababishia matatizo na kuiomba wizara na taasisi zake kuwaandalia mapema mafao yao na barua za kustaafu ili kuangalia upungufu na kurekebisha kabla ya kuwasilishwa katika Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Umma (PSSSF).

Mwakilishi wa watarajiwa hao, Mzamilu Kaita, alisema wastaafu wengi wamekuwa wakicheleweshewa mafao yao kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo ya upungufu unaojitokeza ambao ulipaswa kurekebishwa mapema kabla ya kupatiwa barua za kustaafu, hatua ambayo inasababisha baadhi ya wastaafu kuishi maisha ya kutaabika.

Katika mafunzo hayo yaliyofungwa na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Allan Kijazi, Kaita alisema: "Mheshimiwa Naibu Katibu Mkuu, tunaomba utusaidie katika hili ili tunapostaafu isichukue muda mrefu kupata mafao yetu, ili tusionekane na mabahasha kila kukicha ofisini kwako."

Akifunga mafunzo hayo, Dk. Kijazi aliahidi kulifanyia kazi suala hilo, huku akiwataka wastaafu kushirikiana na wananchi kuibua mtandao wa wale ambao wanajihusisha na ujangili ili kuhakikisha wanafikishwa mbele ya vyombo vya sheria.

Pia aliwataka watumie elimu waliyoipata kwenye utumishi wa umma kupitia wizara hiyo, kuwaelimisha wananchi wenzao ambao hawaelewi umuhimu wa kuhifadhi maliasili.

"Mnapaswa kutoa elimu kulingana na utaalamu wenu wa masuala mbalimbali ya uhifadhi na kwamba elimu mtakayoitoa kwa wananchi itakuwa sehemu ya chachu ya kuhakikisha mikakati tuliyo nayo katika kuhifadhi maliasili zetu inafanikiwa ndiyo maana ya kuwa mabalozi wetu huko," alisema.

Dk. Kijazi ambaye ni Kamishna wa Uhifadhi wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), aliwashauri wanaotarajia kustaafu utumishi wa umma, kuzingatia mafunzo yao na kuwa makini kwenye uanzishaji wa biashara baada ya kustaafu.

Aliwashauri wastaafu hao kutumia wataalamu wazuri na wanaoaminika wanapohitaji kuanzisha miradi ya kibiashara ili kuwa endelevu zaidi kwa manufaa yao.

# Mimea vamizi 69 yatikisa katika hifadhi za taifa

**Na Sanula Athanas**

SHIRIKA la Hifadhi za Taifa (TANAPA), limesema aina 69 za mimea vamizi imeonekana kwenye baadhi ya hifadhi za taifa na kutishia ikolojia ya hifadhi hizo.

Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi wa TANAPA, Godwell Meing'ataki (pichani), alisema jijini Dodoma wiki iliyopita kuwa, mimea hiyo ina athari hasi kibailojia kwa wanyamapori na hata mazingira ya hifadhi zenyewe.



Alibainisha kuwa Hifadhi ya Taifa Serengeti inaongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya mimea vamizi (ina aina 30), ikifuatwa na hifadhi za taifa za Ziwa Manyara, Kilimanjaro, Arusha Saadani.

Hifadhi za Taifa Mahale, Gombe na Mikumi pia zinakabiliwa na baa hilo.

Mhifadhi huyo aliitaja mimea hiyo kwa majina yake ya kitaalamu kuwa ni pamoja na Chromolaena odorata, Caesalpinia decapetala na Acacia zanzibarica.

Alitaja madhara ya mimea hiyo kuwa ni yanajumuisha kusababisha vifo kwa wanyamapori watakaoila.

Kamishna Meing'ataki alisema mimea hiyo inaingia hifadhini kutokana na watu kutupa taka ndani ya eneo la hifadhi, mbegu za mimea hiyo kusafirishwa na upepo hadi hifadhini, wanyamapori wanaobeba mbegu zake wanaporejea kutoka maeneo ya nje ya hifadhi pamoja na mabadiliko ya tabianchi.

Mwezi uliopita, Nipashe ilichapisha ripoti iliyoanika namna utupaji wa taka unavyoathiri ikolojia ya Hifadhi ya Taifa Mikumi (MINAPA).

Wenyeji wa hifadhi hiyo walibainisha kuwa ulifika wakati nyani na tumbili walibadili utaratibu wa mlo, wakawa wanakaa barabarani kusubiri warushiwe chakula na abiria wa magari yanayopita ndani ya hifadhi hiyo badala ya kujitafutia chakula kwenye maeneo yao ya asili.

Tatizo lilionekana kubwa zaidi, wanyamapori hao walipobainika kukariri hadi muda wa mabasi yanayotoka Dar es Salaam kupita ndani ya kipande cha Km 50 za barabara ya lami inayokatiza ndani ya mandhari ya hifadhi hiyo.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO**

**MWALIKO KWA WADAU WA KUSHIRIKI KATIKA SHUGHULI ZA KAMATI YA SERA ZA KODI (TASK FORCE ON TAX REFORM) KWA AJILI YA MATAYARISHO YA BAJETI YA 2021/22**

Kamati ya Ushauri ya Sera za Kodi (Task Force on Tax Reform) inayohusika na matayarisho ya Bajeti ya Serikali 2021/22 itaanza kazi yake mnamo mwezi Februari 2021.

Kamati hiyo ya Ushauri wa Sera za Kodi kwa muda mrefu sasa imekuwa ikifanikisha majadiliano ya masuala mbalimbali yanayohusiana na sera za kodi na usimamizi wake. Mikutano hii imekuwa ikitoa mchango mkubwa kwa waandaa sera kwa muda mrefu. Hali hii imesaidia sana katika kuunda mfumo wa kodi ambao kwa kupitia majadiliano/mazungumzo na uchambuzi umewezesha utatuzi wa masuala mbalimbali ya kodi kwa ufasaha na uwazi

Kutokana na umuhimu huo, Sekretariati ya Kamati itaandaa mkutano wa wadau kwa ajili ya kuwasilisha mada na kuzijadili ambapo Serikali itaongoza mjadala huo kwa kutoa malengo yake ya sera, agenda, changamoto na kutathmini vipaumbele vya sera za mapato katika bajeti ya 2021/22. Hali hii itawapa washiriki mtazamo mpana zaidi kuhusiana na shughuli za mwaka huo na kujadili na kuchambua kwa kina zaidi mapendekezo yatakayotolewa na Serikali pamoja na wadau mbalimbali.

Sera za mapato zinalenga kuboresha mazingira ya kufanya biashara ili kuvutia uwekezaji; kuwezesha ukuaji wa biashara ndogondogo na za kati pamoja na ukuaji wa uchumi endelevu; kuboresha mazingira ya ulipaji kodi wa hiari; upanuzi wa wigo wa kodi na matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika usimamizi wa kodi; kuimarisha usimamizi wa sheria za kodi ili kutatua changamoto za ukwepaji kodi na kupunguza upotevu wa mapato na kuwianisha na kupunguza tozo na ada mbalimbali ili kuboresha mazingira ya kufanya biashara na uwekezaji.

Ili kufanikisha suala hilo, Kamati inakaribisha ushiriki wa taasisi za Serikali, Sekta Binafsi, Asasi Zisizo za Serikali, Taasisi za Dini, jamii ya wasomi, taasisi za utafiti na wataalamu wengine katika sekta ya uchumi kwa kutoa maoni ya kuboresha Sera za Kodi. Vile vile, Kamati inakaribisha mada mbalimbali kwa maandishi kutoka kwa wale wanaopenda kufanya hivyo. Mada hizo hazina budi kuonesha yafuatayo:-

- Biashara, kampuni, taasisi, chama/vyama au makundi ambayo wanawakilisha;
- Mapendekezo ya mabadiliko katika mapato ya serikali yanayotokana na kodi na yasiyo ya kodi, ikiwa ni pamoja na uchambuzi wa sekta, maeneo au aina ya walipakodi ambao wataathirika, na kwa namna gani;
- Makisio ya athari kwenye uchumi na mapato ya serikali katika mwaka huu wa utekelezaji na katika miaka ijayo.
- Sababu na uhalali wa mapendekezo ya mabadiliko kwenye sera za mapato na hususan uchambuzi wa namna ambavyo mapendekezo hayo yataisaidia Serikali kufanikisha malengo yake makuu ya kiuchumi, kodi na kupunguza umasikini.
- Pale ambapo mapendekezo yanapunguza mapato ya Serikali (hata katika kipindi cha muda mfupi), mapendekezo hayo hayana budi yaweke hatua bayana na za kuaminika sambamba na msukumo wa jumla wa sera za bajeti ya Serikali ili kufidia upungufu wa mapato ambao utajitokeza.

Tunatarajia kupata mapendekezo kutoka kwa wadau yatakayowezesha majadiliano yenye tija kati ya Serikali na Wadau.

**Mada zote na mapendekezo yawasilishwe kuanzia sasa hadi tarehe 10 Februari 2021.**

**Wasilisha mapendekezo kupitia anuani ifuatayo:**

**Sekretariati ya Kamati ya Kuboresha Mfumo wa Kodi (Idara ya Sera-Ghorofa ya Pili)**
**Wizara ya Fedha na Mipango,**
**Jengo la Hazina,**
**18 Barabara ya Jakaya Kikwete**
**S.L.P 2802**
**DODOMA.**

**Barua pepe: mathias.kadebe@hazina.go.tz au oliver.ndyali@hazina.go.tz**

**Kwa maelezo zaidi piga simu 0713 694 895 au 0657 558 899.**
**Pia tembelea tovuti yetu: www.mof.go.tz.**

**Tangazo hili limetolewa na:**

**Doto M. James**
**KATIBU MKUU HAZINA**
**Disemba 2020**

# Shule kununuliwa vitabu vya mitaala

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

SHULE 110 za msingi wilayani Ludewa mkoani Njombe, zinatarajiwa kununuliwa vitabu vya mitaala mipya, ili kukuza kiwango cha elimu na kuondokana na changamoto ya wanafunzi kumaliza shule bila kutumia vitabu na wakati mwingine hulazimika kupakua mtandaoni.

Ahadi hiyo ilitolewa juzi na Mbunge wa Jimbo la Ludewa, Joseph Kamonga, wakati alipokuwa akizungumza na walimu wakuu wa shule za misingi zilizopo jimboni humo na kujadili changamoto zinazowakabili zikiwamo za kielimu, ili kuzitafutia ufumbuzi.

Wakizungumza katika mkutano huo, walimu walieleza matatizo yanayowakabili na kusababisha kushika nafasi ya mwisho ikiwamo kutokuwa na vitabu vya kufundishia, wazazi kuwashawishi watoto kufanya vibaya mitihani yao na utoro uliokithiri kwa wanafunzi.

Suzana Kibena, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Ikalo, alimweleza mbunge huyo tatizo la vitabu na kudai kuwa kwa miaka mitatu mfululizo darasa la nne na la saba wanafanya mitihani ya taifa kwa kusoma bila kutumia kitabu cha sayansi.

Kibena alisema serikali inawasisitiza kupakua vitabu hivyo mitandaoni kitu ambacho kwa upande wao inawawia vigumu kutokana na gharama na kutokuwa na fedha za kupakulia vitabu hivyo.

"Tunaambiwa tupakue vitabu mtandaoni na kuvitumia kwa wanafunzi ilhali vitendea kazi hatuna, kama kompyuta, printa na ukisema uende stationary kunahitajika hela ya kufanya hivyo, sisi tunaitoa wapi?" Alihoji Kibena.

Akizungumza baada ya kusikiliza tatizo hilo, mbunge huyo alisema kwa kushirikiana na mwenyekiti wa halmashauri, Wise Mgina, pamoja na walimu kuweka mkazo katika suala hilo, aliahidi kununua vitabu hivyo. "Changamoto zenu nimezipokea na ninaahidi kushirikiana nanyi katika kuzitatua, ili muweze kufundishia katika mazingira mazuri na watoto wa wapigakura wangu waweze kupata elimu bora na itakayowawezesha kufanya vizuri na kukuza kiwango cha elimu wilayani kwetu, nitanunua vitabu pia nitalifuatilia suala hili wizara ya elimu ili kujua kwanini vitabu hivyo havipo," alisema Kamonga.

Naye Ofisa Elimu wa Shule za Msingi wilayani Ludewa, Daniel John, alimwomba mbunge huyo kuzungumza na wananchi wake kuacha tabia ya kuwanyanyasa na kuwadhalilisha walimu kwa kuwa wanafanya kazi kubwa ya kuwafundisha watoto wao.

"Nazungumza haya kwa uchungu sana! Kuna baadhi ya wananchi wamekuwa wakiwadhalilisha walimu wangu na kuwanyanyasa bila sababu ya msingi, walimu tunawafundisha watoto wao katika mazingira magumu halafu bado na wazazi wanatuongezea matatizo, tafadhali sana mheshimiwa mbunge naomba uzungumze na wananchi wako waache kuninyanyasia walimu wangu," alisema ofisa elimu huyo.

Kwa upande wa Mwenyekiti wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT), Mkoa wa Njombe, Shabani Ambindwile, akimwakilisha Katibu Mkuu wa chama hicho taifa, aliwasisitiza walimu wakuu hao kuwa na ushirikiano na kujenga upendo kati yao ili kuhakikisha shule zao zinafanya vyema.

Alisema pamoja na kujenga upendo kati yao pia wanapaswa kutowavumilia walimu wazembe ambao huleta matokeo hasi katika shule zao kuja na matokeo mabaya na anayelaumiwa ni mwalimu mkuu.

"Mimi wakati nafundisha nikiona mwalimu mzembe nilikuwa namtupa kwenye stadi za kazi huko kutamfanya ajifunze na kuongeza juhudi katika kufundishia, japo sina maana nanyi mkafanye hivi ila hakikisheni hamuwafumbii macho walimu wa aina hiyo," alisema Ambindwile.



Vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) wa vikosi vya Makutupora na Nachingwea, wakipakia miche ya mikorosho kwa ajili ya kuwasambazia wakulima wa eneo la Mkiwa, Wilaya ya Manyoni. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# Kalemani atishia kuwafuta kazi watendaji TANESCO

**Na Rose Jacob,** MWANZA

WAZIRI wa Nishati na Madini, Medard Kalemani, ametishia kuwafuta ajira wafanyakazi wa Shirika la Umeme (TANESCO), watakaokiuka maelekezo ya kuwaunganishia umeme wananchi kwa bei elekezi ya 27,000.

Kalemani alitoa kauli hiyo mkoani Mwanza, alipofanya kikao na wafanyakazi wa shirika hilo kilichokuwa na lengo la kuongeza mbinu za utoaji huduma kwa wananchi na kuondoa malalamiko yanayoweza kuepukika.

"Kumekuwapo na tabia za watendaji kuuza nguzo za umeme na kuongeza bei zao za kitapeli, kushindwa kutoa huduma kwa wateja walio umbali wa mita 30, sasa nasema hata mteja akiwa mita 200 kutoka nguzo ilipo apewe umeme kwa bei elekezi, ole wake atakayebainika kumwongezea gharama mteja au kumuuzia nguzo," alisema Kalemani.

Vilevile, Kalemani alitoa agizo hilo kwa mameneja wote wa kanda, mkoa na wilaya kuhakikisha vijiji vyote vya Mkoa wa Mwanza vinaunganishiwa umeme ndani ya miezi 18 na kuwataka kuwa wabunifu wa miradi ya kuzalisha umeme ili kuongeza kipato cha taifa na huduma nzuri kwa wananchi.

Kalemani aliagiza wateja wote wanaodaiwa bili za umeme wakatiwe na hakuna kuangalia taasisi gani, watimize wajibu mpaka watakapo lipa madeni husika, kwa kuwa shirika likiyumba hakuna atakaye laumiwa isipokuwa TANESCO.

"Nendeni mkakate umeme wala msiogope na mteja akilipa nusu mkatieni tena mpaka wamalize malipo, fedha hizo zinahitajika kununua vifaa vya umeme, suala la vishoka hili waratibu wake ni watumishi wa TANESCO maana haiwezekani mkoa mzima uwe na wateja 150,000 wengine wote pesa zao mnaweka mifukoni," alisema Kalemani.

Alitaka watoa huduma wa TANESCO, wapatiwe mafunzo ya kuhudumia wateja ili wananchi wajitokeze kwa wingi na kufurahia huduma ya shirika hilo na kuongezeka kwa wateja ili kuongeza kipato kwa shirika hilo.

Naye Meneja wa TANESCO Mkoa wa Mwanza, Mhandisi Felix Olang, alisema mkoa wake hali ya umeme imeimarika ingawa kuna madeni zaidi ya bilioni mbili.

# Matukio ya moto yaua 62, yajeruhi 74

**Na Mwandishi Wetu**

JESHI la Zimamoto na Uokoaji limesema katika mwaka 2000 lilikabiliana na matukio 1,925 yaliyosababisha vifo vya watu 62 wakiwamo wanaume 45 na wanawake 17.

Taarifa iliyotolewa na jeshi hilo, jana, ilisema baadhi ya matukio hayo ni pamoja na yale ya kuungua kwa majengo ya shule za bweni na kusababisha baadhi ya wanafunzi kupoteza maisha na mali kuteketea.

Pamoja na kusababisha vifo hivyo, taarifa hiyo ilisema matukio hayo ya moto yalisababisha majeruhi 74, wakiwamo wanaume 52 na wanawake 22.

Sababu kubwa za matukio hayo, kwa mujibu wa jeshi hilo, ni uzembe, hujuma na hitilafu za umeme.

"Hata hivyo kwa upande wa shule za bweni tumebaini wanafunzi wanachaji simu kwa kificho kwa kutumia nyaya za umeme zilizopita darini, kutumia 'heater', kutumia pasi bila kuwa waangalifu, mishumaa wakati umeme ukikatika, pamoja na kutumia taa zinazotumia mafuta sehemu ambazo hakuna umeme," lilisema jeshi hilo kwenye taarifa yake.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, jeshi hilo pia lilifanya uokozi katika maeneo mbalimbali zikiwamo ajali za barabarani, mafuriko, kwenye migodi, mashimo ya vyoo, mito, mabwawa na baharini.

Katika uokozi huo, taarifa hiyo ilisema kulikuwa na matukio 845 yaliyosababisha vifo 495 wakiwamo wanaume 402 na wanawake 93.

"Pia maokozi (uokozi) hayo (huo) yalikuwa (ulikuwa) na majeruhi 817 kati ya hao wanaume ni 570 na wanawake 247," ilisema taarifa hiyo.

Jeshi hilo lilisema kutokana na matukio hayo, limekuwa na utaratibu wa kufanya uchunguzi ili kubaini vyanzo na kutoa taarifa kwa umma pamoja na ushauri ili kupunguza kujirudia.

"Baada ya kufanya uchunguzi, baadhi ya maeneo tumetoa maelekezo na kushauri, ili kupata mwarobaini wa tatizo. Hivi karibuni tumekuwa na matukio mengi ya kuungua kwa shule. Shule 44 zimeungua na kusababisha kupoteza maisha kwa baadhi ya wanafunzi, kuharibu miundombinu na kuteketea kwa vifaa vingi," ilibainisha taarifa.

Ili kupunguza majanga ya moto shuleni, jeshi hilo lilisema limeingia makubaliano na Chama cha Skauti Tanzania kutoa elimu kwa wanafunzi baada ya wao kupatiwa mafunzo ya utoaji elimu ya kinga na tahadhari ya majanga ya moto. Katika kufanya hivyo, Zimamoto ilisema skauti watakuwa sehemu ya wazimamoto wa kujitolea na pia jeshi limeanzisha klabu rafiki za Zimamoto katika shule za msingi na sekondari na mpaka sasa kuna klabu 786 zenye wanachama 34,018.

HABARI KITAIFA

# Waziri aiagiza TANROAD kumsimamia mkandarasi

**Na Julieth Mkireri,**
CHALINZE

WAZIRI wa Ujenzi na Uchukuzi, Dk. Leornad Chamuriho, ameutaka Wakala wa Barabara mkoani Pwani (TANROAD), kumsimamia mkandarasi Messers China Railway Seventh Group, anayejenga kituo cha ukaguzi cha pamoja cha Vigwaza, Halmashauri ya Chalinze.

Dk. Chamuriho alitoa agizo hilo jana, baada ya kutembelea kituo hicho na kukagua maendeleo ya ujenzi ambao ulianza Septemba, 2019.

Alisema TANROAD inatakiwa kuhakikisha hakuna ucheleweshaji unaofanywa na mkandarasi huyo tofauti na vikwazo vilivyotokea awali na kusababisha kuchelewa kwa mradi huo.

"Kulikuwa na vikwazo vya saruji, mvua na ugonjwa wa Covid-19, hivi vimepita kinachotakiwa sasa ni kazi ikamilike kwa muda ulioongezwa na hapa mmenieleza hadi mwezi Machi utaanza kufanya kazi," alisema waziri.

Alisema vikwazo vya ucheleweshaji wa fedha za mradi na saruji tayari serikali imevifanyia kazi na kwamba mvua na ugonjwa wa Covid-19 imesababisha mkandarasi huyo kuongezewa muda na kuzingatia makubaliano.

Alisema lengo la ujenzi wa kituo hicho ni kurahisisha ukaguzi wa magari yanayoelekea nje ya nchi, kuhakikisha wanasafirisha mizigo bila bugudha na kwa haraka.

Mhandisi mshauri wa kampuni ya Atkins wa mradi huo wa kituo cha ukaguzi wa pamoja awamu ya kwanza Vigwaza, Isack Shayo, alisema kitakapokamilika kitapunguza gharama za wasafirishaji wa mizigo.

Alisema mradi huo unaotarajia kugharimu Sh. 17,138,219,668.39 kwasasa umefikia asilimia 90 ya utekelezaji.

Alisema mradi wa OSIS Vigwaza haukuweza kukamilika kwa wakati na kwa mujibu wa mkataba kutokana na vikwazo vya uhaba wa saruji, malipo kutolipwa kwa wakati na ugonjwa wa Covid-19.

Shayo alisema ugonjwa huo uliathiri mradi huo kwenye suala la vipuli kutoka nje ya nchi na ajira ya wafanyakazi kulingana na mahitaji ya mradi.

Kaimu Meneja wa TANROAD, Mkoa wa Pwani ambaye ni mhandisi wa matengenezo, Wilicis Mwageni, alisema kituo hicho kitakapokamilika kitakuwa na Taasisi za TRA, Maliasili na nyingine zinazohusika na ukaguzi.

Mwageni alisema kwa sasa magari ya mizigo kwenda nje ya nchi yanakaguliwa katika kituo cha Misugusugu.

# Jafo achukizwa ucheleweshaji miradi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, ameeleza kuchukizwa na kitendo cha ucheleweshwaji wa miradi katika Wilaya ya Chemba, mkoani Dodoma.

Amemwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmshauri ya Chemba, kuhakikisha leo saa nne asubuhi anampelekea maelezo ni kwanini wasichukuliwe hatua kwa uzembe huo.

Miradi hiyo ni ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa na bweni moja katika Shule ya Sekondari Chemba na jengo la utawala la halmashauri hiyo ambayo hadi sasa haina maendeleo licha ya kutakiwa kukamilika ndani ya mwaka huu.

Pia Jafo alikataa kupokea taarifa kuhusu mradi wa ujenzi wa hospitali ya wilaya hiyo ambayo inaeleza uwapo wa upungufu wa fedha wakati serikali imekamilisha fedha yote kiasi cha Sh. bilioni 1.8.

Kutokana na hali hiyo, Waziri Jafo alimwagiza Katibu Mkuu TAMISEMI, Mhandisi Joseph Nyamhanga, kuunda timu maalum ili kuchunguza matumizi ya fedha za miradi katika wilaya hiyo na kazi hiyo ianze Januari mosi, hadi 19, 2021 iwe imekamilika.

"Nimezunguka huko, lakini hapa Chemba mna hali mbaya na hiyo inasababishwa na baadhi ya viongozi kutojua changamoto za wananchi maana hapa kuna watoto wanahitaji huduma, lakini ninyi hamfanyi kazi na ni dhambi kubwa mnafanya. Kutokana na hali niliyoikuta hapa nakuagiza mkurugenzi kesho (leo) saa nne asubuhi, nipate maelezo kwanini msichukuliwe hatua kwa uzembe nilioouona na mnajirekebisha vipi," alisisitiza Jafo.

Alisema, Chemba ni wazembe na wanacheza na fedha licha ya kuwa Rais John Magufuli, ndiye aliyetoa na hiyo inatokana na wengi wao kukulia kwenye mboga nane na hawajui matatizo ya wananchi wa hali ya chini.

Aliongeza kuwa, hawezi kuhangaika kwa watu ambao hawana uchungu na wananchi na kwamba kuna viongozi wamepewa dhamana, lakini hawajui matatizo.

"Kwa sababu haiwezekani hadi leo hamjajenga ndio mmeanza msingi kwa hiyo nataka maelezo kwanini serikali isifanye jambo kwa uzembe huo, mkurugenzi hali niliyoiona pale sijui huko mbeleni.

"Ujenzi wa hospitali za wilaya wenzenu wamefanya mambo makubwa zaidi ya mliyofanya na sijaridhishwa na mmenipa taarifa ya uongo kwamba mmepokea bilioni 1.5 badala ya Sh. bilioni 1.8 ni kosa kubwa," alisema Jafo. Alisema, kati ya halmashauri zote katika jiji la Dodoma Chemba haina uhusiano mzuri na ndio maana kuna matatizo mengi.

"Kila kitu kibaya kipo Chemba, hivi nyie ni watu wa aina gani na niwaambie hii ziara nimekuwa 'very disappointed' kwa hiyo fanyeni tathmini maana uhusiano hapa si mazuri," alieleza Jafo.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Suala la mafao wastaafu lipewe uzito unaostahili

**KWA** muda mrefu kumekuwa na kilio cha wastaafu kucheleweshewa mafao yao, huku sababu za tatizo hilo zikielezwa kuwa ni waajiri kutokuwasilisha makato ya wafanyakazi kwa wakati na upande mwingine mifuko ya hifadhi ya jamii ikitupiwa lawama kuwa ndiyo chanzo.

Licha ya kutupiana mpira kwa waajiri na mifuko, sababu nyingine ambayo hudaiwa kuwa chanzo ni kutokuwapo kwa vielelezo au taarifa kamili kuhusu wafanyakazi. Hali hiyo imekuwa ikisababisha watumishi wa mifuko kuwapiga kalenda watumishi ambazo huambatana na wimbo usio na mwisho wa 'njoo kesho'.

Mambo hayo kwa kiasi kikubwa yamekuwa sawa na donda ndugu na kusababisha wastaafu kuona utumishi wao wa zaidi ya miaka 30 ulikuwa mzigo na mateso kwao kwani hawanufaiki na jasho walilolitoa kwa kipindi chote hicho.

Katika miezi kadhaa iliyopita, baadhi ya wastaafu walikaririwa na vyombo vya habari wakisema miongoni mwao wana miaka miwili hawajapata mafao yao kutoka kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii, huku sababu za kuchelewa huko zikitajwa zile zile za kutokukamilika kwa vielelezo na waajiri kutokupeleka makato.

Kilio kama hicho pia kiliibuliwa wiki hii wakati wa mafunzo ya kujiandaa kustaafu kwa watumishi wa Wizara ya Maliasili na Utalii na taasisi zilizo chini yake. Katika kilio chao hicho, watumishi hao, kwa jina lingine wastaafu watarajiwa, waliomba waajiri kuwaandalia mafao mapema, ili wasisumbuke baada ya utumishi wao kufikia ukomo.

Watumishi hao, yamkini, wamepaza sauti baada ya kuona wenzao waliotangulia wakifuatilia mafao yao baada ya kuondoka kwenye utumishi kwa muda mrefu na bila mafanikio. Huenda watumishi hao wamefikia hatua hiyo kama msemo unenao kwamba "ukiona mwenzio ananyolewa tia maji".

Watumishi hao hawakupepesa macho wala kuficha maneno kwamba hali hiyo imekuwa ikiwasababishia matatizo ikiwamo wengi wao kushindwa kupata haki zao hizo kwa sababu baada ya utumishi wanakwenda kuishi nje ya sehemu walizokuwa wakifanyia kazi. Mtu aliyekuwa akifanyia kazi Dar es Salaam akahamia Bukoba baada ya kustaafu, atakuwa na uwezo gani kifedha kufuatilia mafao yake iwapo kutakuwa na kutupiana mpira kati ya mwajiri na mfuko?


Ni ukweli kwamba watumishi wengi wamekumbwa na mkasa wa namna hiyo na matokeo yake kukumbwa na matatizo ya kiafya kama vile kiharusi na msongo wa mawazo na wengine kupoteza maisha.

Umefika wakati suala hili likafika mwisho kwa kuwaandalia watumishi mazingira mazuri ya kupata mafao yao, ili watakapofikia wakati wa kustaafu, wanufaike na kile walichokitolea jasho kwa muda mrefu.


Hata mifuko ya hifadhi pia inapaswa kuchunguza kwani kumekuwa na malalamiko kwamba baadhi ya maofisa wake wamekuwa wakitumia mwanya wa kuwazungusha wastaafu kwa lengo la kuwapa rushwa ili wayashughulikie madai yao kwa haraka.

Wastaafu wanapaswa kupewa heshima yao kwani wametoa mchango mkubwa kwa maendeleo ya taifa. Kuendelea kuwacheleweshea mafao yao ni kufupisha maisha yao na kuona walichokifanya ni mateso kwao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Yasmine Protace

# Nawakumbusha mlioko famasi, leo mwisho kujisajili mkubalike

**WANAOTOA** dawa za matumizi ya binadamu, pasipo kufuata kanuni na mwongozo mjiandae kujitambua mnajikalisha katika kuti kavu.

Hiyo iko wazi kuna malalamiko mengi kwenu, kwamba kuna baadhi ya watu wanapewa dawa kutoka katika baadhi ya maduka ya dawa na wanapozitumia, wanaangukia matatizo zaidi badala ya kulelekea kupona.

Hili ni tatizo, kuanzia kisheria hadi kitaaluma na hata kijamii. Jibu la kurejea katika usahihi wa kuondoa malalamiko hayo, kinachopaswa kufuatwa ni kuzingatia miongozo itakayomsaidia kila mdau kufaidika na huduma ambazo mgonjwa anazihitaji.

Mara nyingi miongozo imekuwa ikitolewa kwa wahusika waifuatilie na iweze kuwasaidia katika kufanya kazi zao za kila siku.

Kama watoa huduma watashindwa kufuata miongozo, nao hapo wanakuwa wachangiaji wa kuwapo malalamiko ya kila mara.

Hivyo, ili kuondoa malalamiko kutoka kwa wananchi pale wanapotaka huduma ikiwamo upatikanaji wa dawa kinachotakiwa kufanyika ni kuzingatia miongozo ambayo wamepatiwa na mamlaka za afya serikalini.

Uangalizi na umakini unatakiwa kwa kuwapo ajira ya wenye sifa na ndio wanapaswa kuwapo kuhudumia kilicho sahihi kwa dawa za binadamu.

Katika kuhakikisha matatizo hayatokei kwa jamii, serikali inawataka mafamasia, mafundi dawa sanifu na wasaidizi wao nchini, ikiwakumbusha kuhuisha leseni zao leo ni siku ya mwisho, ili kuwawezesha kuendelea kufanya kazi zao za kitaaluma kwa mwaka unaokuja.

Msajili wa Baraza la Famasi, Elizabeth Shekalaghe, amewaambia kwa kukumbusha vifungu vya Sheria ya Famasia, inayowataka kuhuisha majina yao kwenye orodha ya usajili, kwa utaratibu maalumu uliopo.

"Pamoja na Baraza la Famasi kusajili wanataaluma kwa mujibu wa kifungu cha Sheria ya Famasi nchini, kifungu kinatutaka kabla ya tarehe 31 Desemba ya kila mwaka kuhuisha majina ili kuweza kufanya kazi za kitaalamu kwa mwaka unaokuja," amesema.

Kwa upande wa uuzaji dawa, Msajili wa Baraza hilo, Shekalaghe, anawaambia tatizo la uuzaji dawa kiholela limekuwa sugu nchini.

Ni kutokana na hilo, Waziri mwenye dhamana na Afya, Dk. Dorothy Gwajima, ameshaidhinisha kanuni za udhibiti na usimamizi wa uuzaji wa dawa za cheti, hivyo anawataka wanataaluma wafamasi kuhakikisha wanazisoma na kuzielewa vyema.

"Kama wafamasia na wataalamu tukumbuke tuna watu tunawasimamia na kuhakikisha dawa tunazitoa kwa kuzingatia miongozo iliyopo na Baraza halitosita kumchukulia hatua yeyote atakayeenda kinyume na kanuni hizo," anasema.

Mkuu huyo wa Famasia nchini anawataka wananchi kutoa taarifa kwenye baraza hilo, pale wasiporidhika na huduma zitolewazo katika famasi na maduka ya dawa muhimu.

Amethubutu kutoa namba 0736 222 504 au namba bila malipo 0800110015, ili wakabiliane na kasoro wanazokutana nazo wakati wanapatiwa huduma hizo.

Nasema ni hatua nzuri na mfano unapaswa kuingiwa katika vita kukabili upungufu katika sekta ya afya, upande wa utoaji dawa na wakati huohuo, ni namna ya kumuunga mkono kasi yake mpya aliyoanza nayo waziri.

**Katika kuhakikisha matatizo hayatokei kwa jamii, serikali inawataka mafamasia, mafundi dawa sanifu na wasaidizi wao nchini, ikiwakumbusha kuhuisha leseni zao leo ni siku ya mwisho, ili kuwawezesha kuendelea kufanya kazi zao za kitaaluma kwa mwaka unaokuja.**

RIPOTI MAALUM -2

# Shida kuu kijiji kisichokuwa na zahanati kwa miaka 46

- Mkurugenzi Afya: Ni kweli lipo tatizo Masunula
- Akiri haimo katika bajeti, ila chanjo tembezi
- Watumishi afya wapo nusu, wajuzi chanjo 29%

**Na Sanula Athanas, aliyekuwa**
SHINYANGA

**SEHEMU ya kwanza ya ripoti hii jana, ilianika hali ngumu ya upatikanaji wa huduma za afya kijijini Masunula, wakazi wake wakiangukia madhara ya vifo na wanaothubutu kutafuta huduma, wanasafiri umbali mrefu. Endelea kupata ufafanuzi kutoka utafiti wa Nipashe...**

WAKATI hali ikiwa hivyo mkoani Shinyanga, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), anabainisha kuwapo kwa udhaifu katika upatikanaji wa huduma za kinga na chanjo nchini.

CAG, Charles Kichere, anaanika dosari hiyo kwenye Ripoti ya Ufanisi katika Utoaji wa Huduma za Kinga na Chanjo kwa Watoto nchini, iliyowasilishwa bungeni Aprili mwaka huu.

Anasema udhaifu uliobainika ni pamoja na serikali kutoa fedha pungufu katika ununuzi wa chanjo sambamba na uhaba wa watumishi katika vituo vya kutolea huduma.

Kwa mujibu wa CAG, kwa mwaka wa fedha 2018/19, bajeti iliyopangwa ilikuwa Sh. bilioni 30 na kiasi kilichotolewa kilikuwa Sh. bilioni 9.72, sawa na asilimia 32.

"Ufinyu wa utoaji fedha umesababisha uhaba katika ununuzi wa chanjo. Mfano, vituo vya afya sita kati ya 21 vilivyokaguliwa, havikuwa na chanjo yoyote, wakati vituo vitano havikuwa na chanjo ya surua (Measles Rubella) na vituo vinne havikuwa na chanjo ya polio (OPV)," CAG anafafanua.

CAG anabainisha mwenendo wa uchangiaji bajeti ya Mradi wa Utoaji wa Chanjo na Kinga baina ya serikali na wabia wa maendeleo, unaonesha uchangiaji hafifu kutoka kwa serikali kwa miaka minne mfululizo kuanzia 2015/16 hadi 2018/19.

Vilevile, CAG inabainisha katika mwaka wa fedha 2018/19, kulikuwa na uhaba wa watoa huduma za kinga na chanjo kwa asilimia 71 nchini.

Sambamba na hilo, CAG anafichua dosari nyingine ya nchi kukabiliwa na uhaba wa watoa huduma za kinga na chanjo wenye weledi wa kutoa huduma hizo.

Anabainisha watoa huduma 44 kati ya 136 wanaofaanya kazi katika Idara ya Kinga na Chanjo (IVD) katika vituo 21 vilivyokaguliwa, hawana utaalamu wa masuala ya chanjo na kinga.

**ATHARI HASI**

Taasisi ya WAJIBU, katika Ripoti yake ya Uwajibikaji; Ufanisi, Rushwa na Ubadhirifu Katika Sekta ya Umma, 2020, inabainisha utolewaji finyu wa fedha za ununuzi wa chanjo kwa watoto pamoja na uhaba wa watumishi wenye utaalamu wa kinga na chanjo kwenye vituo vya afya, unasababisha athari hasi.


Taasisi hiyo inarejea Ripoti ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Watoto (UNICEF) ya mwaka jana inayoonesha kila siku nchini kuna vifo 270 vya watoto wenye umri chini ya miaka mitano, vinavyotokana na magonjwa yenye kinga na chanjo kama vile kuhara na malaria.

Uhalisia huo unatoa tafsiri kwamba, katika kila saa taifa linapoteza wastani wa watoto 11 wa umri huo kutokana na maradhi yanayoepukika.

WAJIBU inakumbusha kwamba idadi hiyo ya vifo vya watoto inakinzana na Lengo Namba Tatu (3) la Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) linalosisitiza kumaliza vifo vya watoto walio na umri wa chini ya miaka mitano kufikia mwaka 2030.

"Iwapo huduma za chanjo na kinga zitaendelea kupewa fedha pungufu, WAJIBU inaamini kuwa, ni dhahiri lengo hilo halitafikiwa," taasisi hiyo inatoa hadhari.

WAJIBU pia inanyooshea kidole uhaba wa watumishi wenye taaluma ya kinga na chanjo kwamba umesababisha udhaifu katika utoaji wa huduma za kinga na chanjo hususan kwenye vituo vya afya, hivyo kuifanya jamii kukosa huduma hiyo muhimu.




Hali ya utolewaji wa fedha za ununuzi wa chanjo nchini katika miaka mitatu iliyopita. CHANZO: Ripoti ya Uwajibikaji ya Taasisi ya WAJIBU kuhusu Ufanisi, Rushwa na Ubadhirifu Katika Sekta ya Umma, 2020 (Uk. 8).



Mkurugenzi wa Afya, Lishe na Ustawi wa Jamii, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Dk. Ntuli Kapologwe,

**NINI KIFANYIKE**

Ili kutatua tatizo hilo, WAJIBU inashauri Wizara ya Fedha na Mipango itoe kipaumbele kwa bajeti ya huduma za chanjo na kinga, ili kutoa fedha kwa wakati na kwa ukamilifu.

"Wizara ya Afya na Ofisi ya Rais - TAMISEMI (Tawala za Mikoa na Serikali za Mikoa) kwa kushirikiana na Asasi za Kiraia (AZAKI), zitoe mafunzo kwa watumishi wasio na weledi wa kinga na chanjo kwenye vituo vya afya ili kuongeza ufanisi na ubora wa utoaji wa huduma hizo.

"Serikali iweke mkakati maalum wa kuhakikisha inatenga na inatoa fedha husika kama inavyokubalika kati ya serikali na wadau wa maendeleo ili kutowavunja moyo wadau hao," WAJIBU inashauri.

**KAULI YA SERIKALI**

Uchunguzi wa Nipashe ulihamia mezani kwa Mkurugenzi wa Afya, Lishe na Ustawi wa Jamii, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Dk. Ntuli Kapologwe, ili kujua mustakabali wa kinachojiri katika Kijiji cha Masunula na maeneo mengine nchini.

Dk. Kapologwe anakiri kusahaulika kwa kijiji hicho na vingine vya Kata ya Usule katika utekelezaji wa mpango wa ujenzi wa zahanati kila kijiji na kituo cha afya kila kata.

Anataja kiini cha dosari hiyo kwamba kinajumuisha kile alichokiita "upendeleo wa kikundi uliofanywa na baadhi ya viongozi ndani ya Halmashauri ya Shinyanga".

Hata hivyo, Nipashe ilipowasilisha swali hilo kwa mamlaka yenye wajibu wa kuwekeza mradi huo wa zahanati hiyo kijijini, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Hoja Mahiba, alisema mzizi mkuu wa kutokuwapo zanahati miaka yote hiyo 46, ni kukosekana andiko la kuomba msaada wa kujengewa kutoka mamlaka ya kijiji.

Katika ufafanuzi wake, Mkurugenzi wa Afya wa TAMISEMI, Dk. Kapologwe, anasema: "Jimbo la Solwa ni kubwa na tumejenga zahanati nyingi kule, lakini tumebaini ukanda wa kaskazini una zahanati nyingi kuliko kusini, na ndiyo maana maeneo kama ya Kata ya Usule yamesahaulika.

"Sasa, suala hili limeshafika kwetu wizarani, tutalishughulikia. Mwaka huu, tunajenga zahanati 555 nchi nzima, lakini niweke wazi kwamba Kijiji cha Masunula na hiyo Kata ya Usule hawamo kwenye mpango.

"Mwaka ujao, na bahati nzuri kuna fungu tunatarajia kulipa kwa ajili ya ujenzi wa zahanati, tutahakikisha vijiji vya kata hiyo vinaingizwa kwenye mpango."

Kuhusu hoja za CAG, mkurugenzi huyo anarejesha sifa nyumbani kwamba ujenzi wa zahanati 1,198 na vituo vya afya 487 nchini, uliofanywa na Ofisi ya Rais - TAMISEMI katika miaka mitano iliyopita, umeongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za chanjo na kinga nchini.

"Baada ya kubaini kusuasua kwa utoaji wa huduma hizo, tumeamua kutotegemea tu vituo vya kutolea huduma za afya vifanye kazi hiyo, bali tumekuja na utaratibu wa kutoa chanjo kwa huduma tembezi na mfumo wa mkoba.


"Utaratibu huu umetusaidia sana kupandisha kiwango cha utoaji chanjo nchini ambao sasa kwa watoto umefikia asilimia 95," anafafanua.

Mkurugenzi huyo pia anajibu hoja kuhusu nchi kukabiliwa na tatizo la kutokuwa na watumishi wa kutosha wenye weledi wa chanjo na kinga pamoja na serikali kutotoa fedha kikamilifu, akisema:

"Kwa sasa tufanya mafunzo hayo nchi nzima. Kila chanjo mpya inapokuja, tunatoa mafunzo kwa watoa huduma. Fedha za chanjo kwa sasa zinatoka sana na ukumbuke fedha nyingi zinatolewa na wadau wa maendeleo."

Akijibu hoja ya uhaba wa watumishi katika sekta ya afya, Dk. Kapologwe anakiri nchi kukabiliwa na tatizo hilo, akibainisha sasa kuna uhaba wa asilimia 48, ambao kimsingi ni sawa na wastani wa nusu ya watumishi.

Msingi wa simulizi hiyo ndefu kutoka kijijini Masunula, unaanika mustakabali mgumu unaoikabili sekta ya afya kuanzia kada ya watumishi hadi miundombinu katika tafsiri yake pana.




Hali ya uchangiaji wa bajeti ya Mradi wa Chanjo na Kinga kwa miaka minne kuanzia 2015/16 hadi 2018/19. CHANZO: Ripoti ya Uwajibikaji ya Taasisi ya WAJIBU kuhusu Ufanisi, Rushwa na Ubadhirifu Katika Sekta ya Umma, 2020 (Uk. 9).

# Ujauzito 'wayeyuka' mazingira tata

**Na Thobias Mwanakatwe**

MARIAM Mligo (19), mkazi wa Kitongoji cha Iyula wilayani Mbozi mkoani Songwe, anayedaiwa kuwa mjamzito wa miezi tisa, ujauzito wake umepotea katika mazingira tata muda mfupi baada ya kushikwa na uchungu.

Tukio hilo lililotokea Desemba 27, mwaka huu saa saba usiku, limezua taharuki kubwa kwa wakazi wa kitongoji hicho ambao muda wote walikuwa wakimwona akiwa mjamzito.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Iyula A, Mawazo Mwamlima, akizungumzia mkasa huo jana, alisema binti huyo ambaye amelazwa katika Kituo cha Afya cha Iyula, katika mahojiano na viongozi wa serikali, alidai kuwa baada ya kupata uchungu, aliingia chooni kujisaidia.

Alidai akiwa chooni alihisi kama amejifungua mtoto na kutumbukia kwenye shimo la choo na tumbo lake likiwa limepungua hatua iliyomfanya kutoa taarifa kwa wanakijiji ambao waliamua kukibomoa choo kwa lengo la kuokoa maisha ya mtoto aliyedaiwa kutumbukia humo.

Mwenyekiti huyo wa kitongoji alisema licha ya jitihada zilizofanywa na wanakijiji kubomoa choo hicho, hawakufanikiwa kuona mtoto aliyedaiwa na mwanamke huyo kutumbukia humo.

"Juzi, tarehe 28 saa 10 alfajiri, nilipokea taarifa za tukio la mama (Mariam) kujifungua mtoto na kutumbukia chooni baada ya kupatwa na uchungu. Kutokana na hali hiyo, wananchi tulianza kazi ya kufumua choo ili kuokoa kiumbe hicho," alisema.

Aliongeza kuwa mazingira ndani ya choo na kwa mgonjwa mwenyewe usiku ule hayakuonesha kama mwanamke huyo alitoka kujifungua ingawa muda wote mwanamke huyo alionekana kuchanganyikiwa.

"Tulichanga fedha na kutafuta vijana wawili walitoboa choo kama unavyoona tundu hilo, ambapo waliingia ndani na kuanza kutoa uchafu wote bila mafanikio yeyote," alisema.

Mmoja wa majirani wa mwanamke huyo, ambaye alitaka jina lake lihifadhiwe, alidai mimba ya mwanamke huyo ilikuwa imepotea kimazingara.

"Sisi tulikuwa wa kwanza kufika ndani mwake, lakini tulikuta yupo vizuri kabisa kwenye viungo vya uzazi na haikuonyesha kama alitoka kujifungua na unajua kama umefanyiwa ushirikina wa kuibiwa mimba... kinachofanyika unatengenezewa mazingira kishirikina na unaona kama tukio la kweli, ndivyo ilivyotokea," alisema jirani huyo.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Mbozi, Dk. Mponjoli Mwangosi, alithibitisha kumpokea mwanamke huyo na kwamba alifikishwa katika Kituo cha Afya Iyula akiwa katika hali ya kuchanganyikiwa.

Alisema baada ya madaktari kupokea maelezo ya mgonjwa, walifanya vipimo vya awali ili kuona uhalisia wa tukio ambapo vipimo vilionyesha hakuwa na mimba.

"Sayansi ya uzazi iko wazi, mwanamke yeyote akipata ujauzito, ndani ya wiki za awali au akijifungua mtoto salama au bahati mbaya amefariki dunia, mama akifanyiwa vipimo kwa njia ya mkojo itaonyesha, lakini kwa yule mteja wetu vipimo vilionyesha hakuwa na ujauzito," alisema.

Alisema kwa sasa mgonjwa huyo anaendelea na matibabu ya kumweka sawa kisaikolojia na baada ya hapo wataendelea na uchunguzi zaidi kitabibu, ikiwamo kufuatilia historia ya mgonjwa kama aliwahi kuwa na tatizo la afya ya akili.

"Kwenye mambo ya uzazi kwa kinamama, kuna kitu kinaitwa mimba isiyo halisia (Pseucyesis Pregnance). Hali hiyo huwaingiza watu wengi kwenye migogoro ya ndoa na kuibua taharuki wakisema kuna mambo ya kishirikina," alionya.

## Wadaiwa TTCL wapewa mwezi mmoja

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndugulile, ametoa mwezi mmoja kwa wizara na taasisi za umma zinazodaiwa na Shirika la Mawasiliano la Simu (TTCL), kulipa madeni yao ya zaidi ya Sh. bilioni 30.

Dk. Ndugulile alitoa agizo hilo jana jijini Dar es Salaam muda mfupi baada ya kutembelea ofisi za TTCL na kuagiza wadaiwa hao wafanye hivyo kabla ya maeneo yao hayajasitishiwa huduma.

Waziri huo alifika kwenye ofisi za TTCL kwa lengo la kufahamiana na kusikiliza vikwazo vya utendaji vinavyolikabili shirika hilo.

Akizungumza katika ziara hiyo, Dk. Ndugulile alisema wizara na taasisi hizo zipo zaidi ya 20 ambazo zinapaswa kuandikiwa barua na mkurugenzi ili zilipe madeni yake ifikapo Januari 31 mwakani.

"Taasisi zinazodaiwa zote, zinapaswa kulipa fedha hizo zinazotokana na huduma wanayopatiwa ifikapo Januari 31, mwaka 2021. Baada ya hapo, nitachukua hatua ya kusitisha huduma ikiwamo kukata mawasiliano katika maeneo husika," alisema.

Alisema ni muhimu wizara na taasisi hizo kuzingatia suala hilo kwa kuwa shirika linatumia gharama kubwa kujiendesha ikiwamo kuendesha mkongo wa taifa.

Dk. Ndugulile pia alisema serikali imebaini hujuma zinazofanyika katika mkongo wa taifa za baadhi ya watu kuiba nyaya na kwenda kuyeyusha kutengeneza madini ya kopa, jambo ambalo linaisababishia hasara shirika.

"Kuanzia sasa, ninaenda kuongea na vyombo vya ulinzi na usalama kuwaelekeza ikitokea mtu yeyote kakamatwa na hizi nyaya, ana kopa ambayo haijulikani chanzo chake, ataingia kwenye orodha ya wahujumu uchumi," alionya.

Dk. Ndugulile pia alitoa tahadhali kwa watoa huduma za mtandao ambao wanahujumu mitambo ya TTCL, ili isifanye kazi vizuri na kuahidi kuwashughulikia.

"Kampuni zinazoihujumu TTCL ninazijua na sitazitaja, ninawapa taarifa tunajua wanachofanya, hizi salamu ziwafikie, tutawachukulia hatua kali," alionya.

Mkurugenzi Mkuu wa TTCL, Waziri Kindamba, aliahidi kufanyia kazi maagizo yaliyotolewa na waziri huyo.




Ofisa Mwandamizi Huduma kwa Wateja wa Benki ya Exim, Farida Chambo (kulia), akikabidhi zawadi ya simu kwa mmoja wa washindi wa wiki wa kampeni ya 'Chanja Kijanja na Exim MasterCard' ya benki hiyo, Krushant Buhecha, jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Anayedaiwa kuua mtoto kizimbani

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

MTUHUMIWA wa mauaji ya mtoto wake yaliyotokea katika Kijiji cha Mwenge katika kata ya mtina Wilayani Tunduru bMkoani Ruvuma

NEEMA Chama (22) anayedaiwa kumuua mtoto wake, amefikishwa katika mahakama ya wilaya na kusomewa shtaka lake.

Wakimsomea mashtaka, waendesha mashtaka Ernest Machiya na Lameck Sekale, walida mbele ya Hakimu Mkazi Idran Chuvaka kuwa mshtakiwa alitekelza tukio hilo Desemba 24, mwaka huu.

Walidai kuwa alifanya mauaji ya mtoto wake, Rashfod Alli (3) katika kijiji cha Mwenge, Kata ta Mtima, Tunduru mkoani Ruvuma.

Machiya na Sekale walidai kuwa mtuhumiwa alifanya kitendo hicho kinyume cha kifungu cha sheria namba 196 na 197 vya kanuni ya sheria sura ya 16 kama vilivofanyiwa marejea mwaka 2019.

Kuwa kwa vile mahakama hiyo haina uwezo wa kusikiliza kesi za mauaji, Hakimu Chuvaka alimweleza mtuhumiwa kuwa ataendelea kukaa gereza kwa ajili ya kusubiri hadi Januari 3, mwakani kesi yake itakapoletwa mahakamani kwa hutajwa.

Licha ya kutajwa, Hakimu aliagiza kukamilishwa kwa upelelezi wa polisi ili hatimaye kesi ipelekwe kwenye mahakama yenye uwezo wa kusikilisha shauri lake.

Mtuhumiwa anadaiwa kutekeleza mauaji hayo kwa kumpa mtoto soda yenye sumu ya panya ili kupata nafasi ya kwanda kufanya kazi za ndani mkoani Arusha baada ya tajiri ambaye alidai alimtumia nauli na kutoa masharti kuwa hahitaji mfanyakazi mwenya mtoto.

HABARI KITAIFA

## Watakiwa kujali usalama barabarani

**Na Ndalike Sonda,** SIMIYU

JESHI la Polisi Mkoa wa Simiyu kitengo cha usalama barabarani limewataka watumiaji wa barabara hasa wanaoendesha vyombo vya moto kujali usalama wa makundi mbalimbali ya watu na wanyama barabarani.

Hayo yalibainishwa na Ofisa Usalama Barabarani Mkoa wa Simiyu, Koplo Magambo Nyaisa, wakati akizungumza na Nipashe.

Alisema kila kundi lina haki ya kutumia barabara bila bughudha ili mradi afuate sheria awapo barabarani.

Koplo Nyaisa alisema ni vizuri kila mmoja akaheshimu alama na matumizi yote ya barabara kwa kuzingatia sheria za usalama barabarani ili kuondaa ajali mkoani humo.

Alisema Jeshi la Polisi kitengo cha usalama barabarani linafanya kazi ya kusimamia sheria na siyo kutunga sheria na kuwataka watumiaji wa barabara kuzifuata ili kila mmoja atimize wajibu wake.

Kwa upande wake Mrakibu Msaidizi wa Polisi ambaye ni Mkuu wa Usalama Barabarani wilayani Bariadi, ASP Andrew Shayo, aliwataka wananchi kuondokana na dhana potofu walizonazo juu ya polisi ili kuimarisha ushirikiano baina yao.

## Wananchi walalamikia uvamizi wa tembo mashambani

**Na Shaban Njia,** NGARA

WANANCHI wa Kata ya Kasulo, Halmashauri ya Ngara, mkoani Kagera, wamemwomba Mbunge wa Jimbo hilo, Ndaisaba Ruhoro, kutatua kero ya uvamizi wa tembo wanaotoka Hifadhi ya Buligi, wilayani Chato wanaoharibu mazao nyakati za usiku.

Tembo 105 wanadaiwa kuvamia nyakati za usiku kila Jumamosi wakati wa msimu wa kilimo kuanzia mwezi Novemba hadi Aprili na kuufanya uharibifu huo.

Wananchi hao walitoa kilio chao jana kwa mbunge wao wakati wa mkutano wa hadhara wa kuwashukuru kwa kumchagua.

Issa Daudi, Mwenyekiti wa Kijiji cha Kamuli, alisema mashamba yaliyoharibiwa ni ya ndizi zaidi ya hekari mbili, mahindi hekari mbili na mashamha ya maharagwe na uharibifu huo hufanyika kwa nyakati tofauti.

Mtendaji wa Kata ya Kasulo, George Richard, alisema tembo hao wamefanya uharibu wa hekari 10 za mazao ya kibiashara na chakula kwa nyakati tofauti na taarifa za uvamizi huo ameshazifikisha katika Ofisi za TANAPA na Mkuu wa Wilaya ya Ngara.

Mbunge wa Jimbo la Ngara, Ndaisaba Ruhuro, aliahidi kutatua kero hiyo kwa kufikisha suala hilo kwa wahusika.

# Madiwani wapewa mwongozo uundaji bajeti

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MADIWANI na wadau wa kilimo wametakiwa kuwa na mtazamo wa haki za binadamu na kushiriki katika mchakato wa maendeleo kwa kuzingatia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, miongozo ya serikali kupitia Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), fursa, vikwazo na uundaji wa bajeti kuwasaidia wakulima wadogo kupata mafanikio chanya katika shughuli zao.

Wakiwasilisha mada kwa nyakati tofauti katika mafunzo wa madiwani na wadau wa kilimo Wilaya ya Mvomero, Mkoa wa Morogoro, Venance Mlali na Dk. Albinie Marcossy, walisema nafasi ya madiwani ni kubwa katika kutatua changamoto zinazowakabili wakulima kupata maendeleo kwenye sekta ya kilimo.

Mafunzo hayo kwa madiwani yaliandaliwa na Mtandao wa Wakulima Wadogo Tanzania (MVIWATA), kwa kushirikiana na Mtandao wa Wakulima Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika (ESAFF).

Kwa upande wake, Venance Mlali wa Asasi ya Mafiga Women, alisema kuwa ili mkulima mdogo aweze kupata haki yake hana budi kuzingatia malengo ya kimataifa kwa kuzingatia lengo namba moja na namba mbili la haki za binadamu kushiriki kwenye mchakato wa maendeleo kwa kuzingatia Katiba ya nchi.

"Kiini cha yote ni mfumo wa uwajibikaji ili kupata matokeo chanya kwenye sekta ya kilimo kujua bajeti za halmashauri ambayo ndio msingi wa kufanikisha kukabiliana na umaskini na njaa," alisema Mlali.

Kwa upande wake, Dk. Albinie Marcossy, alisema mpango wa maendeleo ya taifa na programu ya miaka mitano ya kuendeleza sekta ya kilimo awamu ya pili yenye maeneo mahususi katika mfumo wa utekelezaji na ufuatiliaji kuanzia ngazi ya kijiji hadi ofisi ya Waziri Mkuu, umebebwa na msingi wa uwajibikaji wa jamii, viongozi wa umma wakiwamo madiwani.

Irene Liborious, Ofisa Mradi wa ESAFF, alisema madiwani katika masuala ya uwajibikaji na ushiriki wa wakulima katika sekta ya kilimo ni suala mtambuka katika utekelezwaji nchini Tanzania kwa kuzingatia mipango ya kimataifa na Afrika (CAADP), kuhusu usalama wa chakula.

Naye mwakilishi kutoka MVIWATA, Theodora Pius, alisema taasisi hiyo imekuwa ikiwasogezea wakulima wadogo huduma kwa msingi wa ushawishi na utetezi kwa kufanikiwa kujenga soko la nyandira, kutoa mafunzo kwa wakulima ili kuendesha kilimo chenye tija.

Alisema kwa mwaka 2020 taasisi hiyo kupitia uanachama wake na taasisi ya ESAFF, imefanikiwa pia kuendesha mafunzo kwa wanachama wake kwa kuwashirisha viongozi wa serikali kupitia mfumo shiriki ambao umeleta mafanikio makubwa wanayojivunia.



Katibu Tawala Mkoa wa Morogoro, Emmanuel Kalobero, akishiriki kuchimba msingi kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya ya sekondari ya sayansi katika Kata ya Boma, Manispaa ya Morogoro, itakayokuwa ya ghorofa yenye vyumba 25 na kuchukua wanafunzi zaidi ya 500, pindi itakapokamilika. Kushoto ni Ofisa Elimu mkoani humo, Joyce Baravuga. **PICHA: FRANK KAUNDULA**

# Wanaohatarisha amani, usalama waundiwa mikakati

**Na Tiganya Vincent,**

TABORA

WAJUMBE wa Kamati ya Usalama Mkoa wa Tabora wametakiwa kuendelea kushirikiana kuchukua hatua dhidi ya watu wanaotaka kuhatarisha amani na usalama, ili wananchi waendelee kuwa na mazingira mazuri ya kushiriki shughuli za maendeleo.

Kauli hiyo imetolewa jana na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Elias Kwandikwa, wakati alipokutana na Kamati ya Usalama alipokuwa katika ziara mkoani humo.

Alisema watu wote ambao ni wahalifu ni vyema wakachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria bila kuwaonea huruma.

Kwandikwa aliagiza Kamati ya Usalama ihakikishe inachukua hatua za kuziba mianya yote ambayo inaweza kusababisha uhalifu wa aina yoyote.

Alisema mianya ya uhalifu isipozibwa mapema inajenga mazoea na kuwafanya wananchi kuwa na hofu hata za kutafuta mali.

Kwandikwa aliongeza kuwa wakati mwingine uhalifu katika jamii inakumbwa na kasumba ya undugu na kulindana, huku jamii nyingine zinaendelea kumia na matokeo yake.

Alisema wataalamu wizara anayoiongoza wataendelea kushirikiana na wizara nyingine kuwahakikishia amani na usalama wananchi kwa ajili ya kuwawezesha kufanya shughuli mbalimbali bila hofu.

"Uhalifu unapozidi wananchi wanashindwa kuwekeza kwa hofu kwamba wakipata fedha... wapo watakaokuja kuzichukua," alisema.

Kwandikwa alisema ushirikiano ni muhimu kupambana na wahalifu kwa kuwa watu hao hawatoki mbali bali katika jamii na wakati mwingine baadhi ya familia zisizo na uzalendo zinawaficha.

Kuhusu suala la uhalifu ambalo hujitokeza katika Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori ya Isawima wilayani Kaliua, aliwataka kuangalia njia bora ya kukomesha tatizo hilo.

## Wananchi Ubungo wanililia DAWASA ukosefu wa maji

**Na Vincent Mpepo,** OUT

WAKAZI wa Kwembe kwa Mnoli wilayani Ubungo jijini Dar es Salaam, wameilalamikia Mamlaka ya Majisafi na Majitaka (DAWASA) kutokana na ucheleweshaji wa upatikanaji wa huduma hiyo muhimu. Kwa nyakati tofauti juzi na jana, wakazi hao walidai ukosefu wa maji katika mtaa huo umekuwa kero ya muda mrefu na iliyokosa ufumbuzi licha ya ahadi mbalimbali za viongozi wa siasa na watendaji wa mamlaka husika.

Mwajuma Athuman, mkazi wa mtaa huo, alisema tatizo la ukosefu wa maji ni la muda mrefu na limekuwa likifuatiliwa kwenye mamlaka husika mara kwa mara bila mafanikio licha ya ahadi za kutekelezwa. Alisema umefika wakati wanategemea maji ya mvua kwenye madimbwi ambayo siyo safi na salama kwa afya ya binadamu.

"Tunaishi kwa kutegemea mvua ili tupate maji na ikiisha tunahangaika kununua kwa wanaoleta maji kwa magari, maji ambayo ni ya gharama kubwa," alilalama Mwajuma. Esther Bukagile, mkazi mwingine wa mtaa huo, alisema juhudi za kuomba maji serikalini zilianza miaka ya 1980 na zimeendelea mpaka leo japo kwa miaka ya hivi karibuni mamlaka husika zimedai kuna ukosefu wa mabomba.

"Jambo la ajabu ni kuwa baadhi ya mitaa jirani na mtaa wetu inapata mabomba na wana maji. Kulikoni sisi?" Esther alihoji.

Mbunge wa Kibamba, Issa Mtemvu (CCM), alisema anafuatilia kwa karibu utatuzi wa kero hiyo matatizo mengine yanayowakabili wananchi jimboni kwake.

Aliwataka wananchi waendelee kuwa na subira kwa kuwa atahitaji kufanya mazungumzo na viongozi wa ngazi mbalimbali ili kupata taarifa za utekelezaji kwa kipindi kilichopita na mikakati iliyopo kwa sasa. "Niwaombe wawe wavumilivu wakati tukisubiri utatuzi wa kero hizo kwa kuwa tunahitaji kupata ufumbuzi kwa kushirikisha viongozi wa mitaa husika," alisema Mtemvu. Alisema atakuja na mkakati wa utatuzi wa kero mbalimbali ikiwamo za miundombinu na huduma kwa kushirikiana na viongozi na wananchi wa maeneo husika.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Kwembe, Barnabas Asenga, alisema kulikuwa na tatizo la kiutawala katika nyakati zilizopita, lakini kwa kasi ya utawala huu, mambo yatakuwa mazuri.

"Kulikuwa na shida ya upatikanaji wa vifaa kama mabomba kwa wakati uliopita, lakini kwa awamu hii mambo yataenda vizuri," alisema Asenga.

# Jeshi laandaa miche 300,000 mikorosho

**Na Renatha Msungu,** MANYONI

JESHI la Kujenga Taifa (JKT), limewataka wananchi kujitokeza kununua miche ya kisasa ya mikorosho inayozalishwa na jeshi hilo eneo la Mkiwa wilayani Manyoni mkoani Singida.

Katika eneo hilo Kikosi cha JKT Mkiwa, kimezalisha miche 300,000 kwa ajili ya kuiuza kwa wananchi pamoja na halmashauri ambazo zina uhitaji wa miche kwa ajili ya kupanda katika mashamba yao hususani kipindi hiki cha msimu wa mvua.

Uzalishaji huo umekuja baada ya utafiti kuonyesha kuwa kuna mikoa 17, ukiwamo wa Singida, zao hilo linastawi na kutekeleza mpango wa serikali wa kuimarisha mazao ya kimkakati.

Kufuatia mpango huo, JKT wameamua kuunga mkono juhudi za serikali kwa vitendo katika kuzalisha miche na kuiuza kwa wananchi kwa bei nafuu ili walime zao hilo.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Luteni Kanali Festo Mbanga, Kaimu Kamanda wa Kikosi 834 JKT Makutupora, alisema kuwa kati miche 300,000 ilyozalishwa, tayari 100,000 imechukuliwa na mradi wa Manyoni, huku miche 50,000 ikitarajiwa kupelekwa mradi wa Ikungi na miche iliobaki itakuwa kwa ajili ya kuwauzia wananchi wa eneo la Mkiwa ambao lina uhitaji wa mbegu za korosho.

"JKT baada ya kuona zao hilo linastawi na kuna uhitaji wa mbegu, iliamua kuanzisha vitalu vya miche ya kuzalisha mbegu ili kuunga mkono juhudi za serikali za kuimarisha mazao ya kimkakati.

"Tunawakaribisha wananchi wajitokeze kununua miche ya mikorosho kutoka JKT kwa sababu ina ubora unaotakiwa kwa mkulima," alisema Luteni Kanali Mbanga.

Alisema miche hiyo ina ubora wa hali ya juu ambao utamwezesha mkulima kupata faida kubwa pale watakapopanda na kuihudumia vizuri katika mashamba yao.

Luteni Kanali Nyagalu Malecela, Kamanda wa Kikosi 843 JKT Nachingwea, alisema miche ya korosho iliyopandwa imefanyiwa utafiti na kubaini inafaa kupandwa katika maeneo ya ukanda huo.

Alisema mbegu hiyo inatumia muda wa miaka mitatu tangu kupandwa hadi kuvunwa, hivyo wakulima wanapaswa kuchangamkia fursa ya kununua miche ya korosho ambayo imezalishwa kisasa na JKT.

Alisema jeshi hilo lina uwezo wa kuzalisha miche ya kutosha katika mikoa ambayo zao hilo linastawi.

Alisema wamekuwa wakizalisha miche kila mwaka kwa lengo la kusaidia wakulima mbegu kwa ajili ya kupanda korosho kwa kiasi kikubwa.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Uwekezaji), Prof. Kitila Mkumbo (kushoto), akimsikiliza Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo TIB, Charles Singili (kulia), wakati alipotembelea benki hiyo, ili kuangalia fursa zinazopatikana ili kuweza kuchagiza shughuli za uwekezaji hapa nchini. Katikati ni Mwenyekiti wa Benki ya Maendeleo TIB, Dk. Maria Mashingo.

# Mbunge atekeleza ahadi zahanati kuunganishwa huduma ya umeme

**Na Mwandishi Wetu**

MBUNGE wa Makete, Festo Sanga (CCM), ametekeleza ahadi yake aliyoitoa wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu kufunga umeme jua katika Zahanati ya Kijiji cha Ilindiwe, Kata ya Mang'oto jimboni huko.

Alitoa ahadi hiyo kutokana na wananchi kukosa baadhi ya huduma usiku huku wahudumu wa afya wakilazimika kutumia tochi kutoa matibabu.

Akikabidhi huduma hiyo jana, Sanga alisema wakati akiomba kura wananchi hao, walimwambia adha wanayoipata ya kukwama kupata baadhi ya huduma usiku.

"Nilipokuja mliniambia hitaji lenu la kwanza ni umeme wa jua kwenye zahanati yenu hii, mlihitaji umeme kwa sababu huduma nyingi zinakwama nyakati za usiku na hata zile zinazohitaji umeme.

"Zahanati hii inategemewa na sehemu kubwa ya wananchi wa Mang'oto, nimeona ni vyema nikaitekeleza mapema ili mama zetu wanapohitaji huduma ya uzazi waipate saa zote pakiwa na umeme," alisema.

Mbunge huyo alisema hatua hiyo itawaondolea adha wahudumu wa afya ya kutumia tochi kuhudumia wananchi nyakati za usiku.

"Ninawaomba mzitunze 'solar' hizi ili zitusaidie kwa muda mrefu wakati tunahangaikia umeme wa REA," alisema.

Baadhi ya wananchi walioshuhudia utekelezaji wa ahadi hiyo, walisema wamefurahishwa na namna mbunge wao alivyotekeleza ahadi hiyo kwa haraka kwa kuwa kwa muda mrefu walikuwa wakiwasilisha kilio hicho kwa viongozi mbalimbali akiwamo Mkuu wa Mkoa wa Njombe na viongozi wengine wa kitaifa.

"Huyu Sanga ametupa matumaini makubwa sana sisi wananchi wa Ilindiwe, tunamwombea kwa Mungu ambariki kwa pale alipotoa kwa ajili yetu," alisema mmoja wa wananchi aliyejitambulisha kwa jina la Sara.

ama
ALHAMISI DESEMBA 31, 2020
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12, 13

**Idadi ya wakimbizi wanaokimbia vifo inavyoongeza hesabu wakazi**



Ukurasa 14

**Operesheni ya lishe bora kutokomeza udumavu wa watoto mkoa Shinyanga**

# Dk. Gwajima aanza na kuchokonoa vikwazo kwa wagonjwa vituo afya

- Jicho katika bajeti, maelekezo yaja
- Manaibu wake na mahali pa kupitia

**Na Yasmine Protace**

NI hivi karibuni Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, mjini Dodoma alikutana na wadau wa afya nchini kujadilli mengi yanayohusu sekta hiyo, ikijumuisha upatikanaji dawa katika vituo vya afya.

Kiongozi huyo mgeni katika Baraza la Mawaziri, lakini mkongwe katika ngazi ya juu ya utendaji katika sekta hiyo ya afya, anataja wigo wa kasoro unazama katika maeneo kama kukaa mbali na malalamiko ya kukosekana katika maeneo ya tiba.

Rai ya waziri yenye sura ya agizo, ni kwamba viongozi wa vituo vya kutoa huduma za afya vya umma, wanapaswa kuheshimu mpangilio wa fedha za bajeti ya dawa, ili kuondoa kero ya kukosekana dawa vituoni.

Waziri Dk. Gwajima, katika Mkutano wa 21 wa Kutathmini Utekelezaji Vipaumbele vya Kisera katika Sekta ya Afya jijini Dodoma, anasema bado kuna maoni mengi kutoka kwa wananchi kuhusiana na ukosefu wa dawa na huduma za afya kwa jumla.

Rai yake ni kwamba, viongozi wa hospitali na vituo vya kutoa huduma vya umma nchini, wanapaswa kuainisha matumizi ya fedha za dawa walizopokea au kutoka kwenye makusanyo ya mapato ya hospitali hiyo, pamoja na matumizi yake.



Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima. **PICHA: MTANDAO**

"Ili kufikia azma ya Rais, sisi kama sekta ya afya inabidi kuongeza kasi katika uwajibikaji wa pamoja katika malengo tuliyoyaweka," anatamka na kufafanua:

"Ni lazima tufanye upekuzi wa matumizi ya fedha za dawa, vifaa na maabara, lazima ziheshimike na kufika kwa mgonjwa, ili wananchi watuamini na kuweza kutatua kero zao."

Anasema, katika utekelezaji huo, wizara itatoa maelekezo yanayolenga kuongeza ufanisi kwa watumishi wote wa sekta ya afya, ngazi mbalimbali za usimamizi na uendeshaji wasekta na taasisi zilizo chini ya wizara, pamoja na wadau wote husika wa afya.

Dk. Gwajima anawahimiza wadau wote kuweka kipaumbele kwenye utekelezaji unaozingatia vipaumbele vilivyowekwa na serikali kwa miaka mitano ijayo, yaani mwaka uliopo hadi 2025.

Ni uwajibikaji unaojikita katika utoaji huduma za afya nchini na kuziboresha ili kuwafikia wananchi wote na kuwapatia huduma kulingana na mahitaji ya kiafya yanayowakabili.

Anataja kuwapo kundi kubwa la wananchi walio nje ya mfumo wa bima ya afya, hivyo wanazikosa huduma za afya kwa wakati. Hadu sasa kunatajwa ni asilimia 11 tu ndio wamejiunga na mfumo huo.

Dk. Gwajima anasema zimekuwa zinasaidia katika kutibu magonjwa mbalimbali kwa wananchi, hivyo serikali inakusudia kuimarisha kitengo cha utafiti wa tiba mbadala.

**WANAJIPANGAJE?**

Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais (TAMISEMI), Dk. Festo Dugange, anasema kunahitajika mkakati makini wa kuimarisha mifuko ya bima ya afya, ili iwafikie wananchi wengi zaidi.

Dk. Dugange anataja njia mojawapo ni kukamilishwa mpango mkakati wa Sera ya Ugharamiaji wa Huduma za Afya, pamoja na ujio wa Sheria ya Bima kwa Wote.

"Mfuko wa Afya ya Jamii uliboreshwa kwa sasa unachangia asilimia tano ya wanufaika wote waliojiunga katika mifuko ya bima za afya nchini.

"Katika kipindi cha utekelezaji wa mfuko wa afya ya jamii iliyoboreshwa kuanzia Julai 2018, tumefanikiwa kusajili kaya 557,882 sawa na wanufaika 3,347,112 kufikia Novemba 2020," anasema.

Anasema tayari shilingi bilioni 16.2 zimeshakusanywa kutoka mwaka 2018 hadi mwaka huu, hata ikawezesha kuimarisha huduma za afya kwenye vituo vinavyotoa, jambo linalowawezesha wananchi na makundi maalum kufikiwa, pasipo vikwazo vya fedha.

Naibu Waziri anayehusika na Afya, Dk. Godwin Mollel, anadokeza uwezekano wa sekta ya afya kufanya vizuri, iwapo viongozi na wadau wa maendeleo wa sekta hiyo watajipanga na kushirikiana katika kufikia malengo yanayowahakikishia Watanzania huduma bora za afya.

Dk. Mollel anasema kunahitajika uelewa kuhusu bima kwa ujumla, kwani hadi sasa wananchi wahitaji wengi bado hawajafikiwa, sehemu ya nchi kikuu ni kutokana na mfumo duni wa mawasiliano ndani ya sekta.

Rai yake kwa waganga wakuu wa mikoa, wilaya na waganga wafawidhi wa hospitali kutoa mawasiliano yao, ili wananchi waweze kusaidiwa.

Suala la kikwazo cha mawasiliano katika sekta ya afya, kiliwahi kutolewa katika moja ya ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), katika suala la utekelezaji Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Afya (MMAM).

MAZINGIRA

# IDADI YA WAKIMBIZI WANAOKIMBIA VIFO INAVYOONGEZA HESABU WAKAZI

## •Ina mzizi mrefu kuanzia zama ukoloni
## •Rekodi mauaji kimbari 1994 haishikiki
## •Mkasa 'alivyolala mbele' hadi Kigoma



Wakimbizi wa kambi ya Nduta, iliyopo Kibondo, Kigoma wakimsikiliza Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (hayupo pichani) alipowatembelea.

**Na Christina Mwakangale**

ZAIDI ya asilimia moja ya watu duniani ni wakimbizi, ripoti ya Umoja wa Mataifa (UN), inadokeza.

Hadi sasa ni takriban watu milioni 80 duniani kote wanalazimika kuyahama makazi, kutokana na machafuko na vita.

Tanzania inaelezwa ilianza kupata wakimbizi zaidi ya miaka 60 kabla ya uhuru kutoka nchi tofauti na historia ya tukio la mwaka 1994 nchini Rwanda, iliendana na tukio la wastani wa wakimbizi 250,000 kuvuka drajani la Rusumo mkoani Kagera, kuingia nchini.

"Haijawahi kutokea duniani kokote watu kuvuka mpaka kwa saa 48 zaidi ya laki mbili, kulikuwa na kambi ambayo ilikuwa kubwa kuliko hata mkoa wa Dar es Salaam ulivyokuwa wakati huo.

"Sababu ilikuwa na takribani watu 700, 000," anasema Ofisa Tawala Mkuu, Usimamizi wa Kambi na Makazi kutoka Idara ya Huduma kwa Wakimbizi," anasema, Ofisa Wakimbizi, Stephen Msangi.

Anasema Tanzania inazungukwa na nchi nane, baadhi zilikumbwa na machafuko ya kisiasa yaliyosababisha wakazi wake kuhama. Pia, kuna nchi wakimbizi wake walitokana na waliotambulika kuwa wapigania uhuru.

Katika hizo, kuna Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Burundi, Rwanda, Msumbiji, Malawi, Kenya na Uganda,

Msangi anasema, taifa limeshapokea tuzo za kutunza wakimbizi, ikiwamo medali ya Nansen aliyokabidhiwa Rais Julius Nyerere, jijini Geneva, Uswisi, Oktoba 3 mwaka 1983.

Pia, anamtaja marehemu Rais Benjamin Mkapa, alishapokea tuzo la kuwajali wakimbizi.

### HISTORIA YA WAKIMBIZI

Msangi anaeleza, Tanzania ilianza kupokea wakimbizi kwa awamu mbili tangu miaka ya 1950 hadi 1980, waliikuwa wakitafuta makazi.

"Tulianza kuwapokea hata kabla ya mwaka 1960, wengine waliletwa kutoka Poland, historia inasema hivyo, ingawa haijawekwa sawasawa. Pia, wakimbizi wa Maumau kutoka Kenya na wapigania uhuru," anasimulia Msangi.

Anarejea historia, kwamba awamu za wakimbizi zilikuwa mbili, ikianza miaka ya 1950 hadi 1980, zikipewa jina analolitaja 'settlement base' yaani kambi za makazi, mahali ambako wakimbizi waliruhusiwa kulima na kufanya shughuli nyinginezo, ambazo sasa hawaruhusiwi.

"Waliokuja kwa wingi miaka hiyo hapa nchini na kukaa Warundi, wa -Rwanda, Wa-Msumbiji na kutambuliwa kama wakimbizi, wakiwamo wapingania uhuru. Pia, tulikwa na Waganda, Waafrika Kusini walikuwa na makazi yao," anasema Msangi.

### AWAMU YA PILI

Msangi anaeleza, hiyo ilianza miaka ya 1990, serikali ilipoweka sera na iliamuliwa mwaka 1993 kusiwapo kambi za makazi kutokana na mfumuko wa wakimbizi.

Anasema takribani miaka 10 kati ya 1990 hadi 1998, Tanzania ilipokea kiasi kikubwa cha wakimbizi, rekodi ambayo haijawahi kufikiwa.

"Wakimbizi wengi waliingia kutoka Burundi baada ya kifo cha Melkiori Ndadaye na ikaamuliwa kuwe na kambi tu, yaani wakimbizi wakae kambini," anasema Msangi.

Pia, anasema tukio la mauaji ya kimbari nchini Rwanda, ambako takribani watu 800,000 walipoteza maisha, ilisababisha kuongezeka wakimbizi nchini.

Msangi anaeleza: "Zaidi ya watu 700,000 waliingia Tanzania wakati katika kipindi hicho watu 250,000 walivuka mpaka katika daraja la Rusumo (Kagera) kwa saa 48,"

Aidha, anasimulia kati ya mwaka 1996 na 1998, kulikuwapo na wakimbizi wengi kutoka DRC, baada ya vita ya ndani kumpindua serikali ya Rais Mobutu Seseko, huku rekodi hiyo ya wingi ilianza kwa muakia 10 tangu mwaka 1990.

Msangi anasema mwaka 2015, ulikuwa na mazito yake, wakimbizi Warundi 200,000 walivuka mpaka kuingia nchini kutokana na vita ya kisiasa katika uchaguzi,

Anaeleza, serikali ililazimika kuondoa sera ya wakimbizi kuruhisiwa kulima mashamba makubwa na kumiliki ardhi, badala yake wakawa wanapokea vyakula, huduma za afya, elimu na nyinginezo wakiwa kambini.

Msangi anasema, pia ni uamuzi ulioelekeza kambi zote ziwe jirani na mipaka, ili pale inapopatikana amani iwe rahisi kurudi nchini mwao.

Anasema kwa miaka 29, tangu 1964 hadi 1993, Shirika la Kuhudumia Wakimbizi, Tanzania Centre for Refugees Services (TFRS), lilikuwa maalum kwa ajili ya kuhudumia wakimbizi, ikiwamo mahitaji kama maji na baadaye yaliongezeka mashirika ya huduma kama hizo, ikiwamo Msalaba Mwekundu.

"Hadi sasa tuna wakimbizi takribani 200,000 ambao wengi wao ni Wacongo. Takwimu kuanzia Mei mwaka huu ni kwamba, tuna mataifa kadhaa ambao tunawahifadhi wenye 'status'(hadhi) ya wakimbizi kama vile Wasomali, Wa- Ethiopia, Madagascar, Wakenya, Wazimbabwe, Waeritrea, Wa-Yyemen, Wa - Syria, Lebanon, Madgascar, Uganda na Comoro

### MIKATABA KIMATAIFA

Ofisa huyo anasema, Tanzania imetia saini mikataba ya kimataifa na inasimamia utoaji huduma za kijamii kambini, akieleza: "Mfano, ili mtu a'-survive' (aishi) au aliye na afya anahitaji kalori 2100.

"Kwa hiyo anachohitaji mtu mmoja ni unga wa ugali gramu 350; unga wa uji gramu 50; maharage gramu 120; chumvi gramu tano na mafuta gramu 20 kwa siku. Kazi yetu ni kusimamia hicho wanachopata wanapewa.

"Mkuu wa kaya anakuwa mwanamke katika kambi, vilevile tunasimamia hata utoaji sabuni, ingawa kuna wakati hakuna ufadhili, baadhi ya vitu havipatikani," anasema Msangi.

Pia, Msangi anasema mafanikio kwa nchi ni kusimamia kurejea kwa wakimbizi na tayari wakimbizi milioni 1.3 wamerejea kwao, kutoka Burundi, Rwanda na DRC.

"Wakimbizi waliokwishapewa uraia wa Tanzania, 162,106 hii ilikuwa mikaa ya 1980 na 1993."

Bila ya kufafanua, anaeleza Tanzania imewapeleka katika nyinginezo anazozitaja 'nchi ya tatu' jumla ya wakimbizi 40,000 na hadi sasa impokea tuzo kadhaa, ikiwamo ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR).

Penye mafanikio pana magumu, Msangi akigusia magumu yaliyopo katika maeneo ya wakimbizi, ikiwamo usalama mdogo akijumuisha kuwapo wizi, umiliki wa silaha kiholela na mazingira kuharibiwa.

Anatoa rai ya haja namna ya wadau wakaangalia kuwezesha matumizi mbadala ya nishati ya kupikia maeneo ya kambi, ikiwamo gesi na mkaa mbadala kunusuru mazingira.





Wakimbizi kutoka Burundi katika kambi ya Nyarugusu, Kigoma wakiwa wamebeba unga na mahindi, baada ya kugawiwa chakula hicho na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Chakula (WFP), lililoweka kituo chake katika kambi hiyo, Nyarugusu wilayani Kasulu.



Raia wa Burundi wakiandikishwa kabla ya kusafirishwa kupelekwa katika kambi ya wakimbizi ya Nyarugusu, wilayani Kasulu, Kigoma. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU**



Raia wa Burundi wakiwasili eneo la Bandari ndogo ya Kibirizi, katika Manispaa ya Kigoma Ujiji, mkoani Kigoma.

### SIMULIZI YA MKIMBIZI

John Ebengo, mkimbizi msomi mwenye shahada ya uzamili katika lugha ya Kifaransa, akitokea nchini DRC, anasimulia maisha yake ni mwalimu anayefundisha katika shule binafsi.

Ibengo, pia anajitambulisha ni Mchungaji wa Kanisa la New Apostolic Church, anaishukuru serikali kumpatia kibali cha kuishi nje ya kambi na kufanya kazi.

"Huwa nawaambia ndugu zangu wakimbizi, tusifuate habari za mitaani. Sheria zilivyo zimesaidia mimi kuajiriwa maeneo tofauti. Ukifuata utaratibu wa vibali, Uhamiaji, Shirika la Wakimbizi, pia utaweza kuishi.

"Ukiomba kibali cha kufanya kazi, utapata iwapo itakuwa na vielelezo vya huko unakotaka kufanya kazi. Nilifuta utaratibu huo na shule inanihitaji kufanya kazi, nikapata fursa ya kazi," anasema Ebengo.

"Nilikuwa nakaa kambini Nyarugusu, nikamuwona mwenyekiti katika kambi ili kuomba kibali cha kupata kazi nje ya makazi ya kambi.

"Niliitwa na shule ya Misheni ya Kikatoliki, pia nikaenda Shirika la Asylum Access, hivi sasa Dignity. Kwanza, nikaonyesha kibali, wakasema niende Wizara Mambo ya Ndani 'document' (nyaraka) zangu nilizipeleka huko."

### MKASA WA 1996

Ebengo anasimulia tukio la Oktoba 25, alikuwa mtumishi wa serikali na kila baada ya saa sita, walikuwa wanapeleka ripoti katika maeneo tofauti, pasipo kuelewa undani wake. Hata hivyo, walishangaa milio ya risasi na watu wakikimbia kila mahali.

"Nimeingia Tanzania mwaka 1996, Novemba 3, nikiingilia Kigoma, katika hilo kundi linalozungumziwa 200,000, mimi ni mmoja wao, nikitoka hivi nilivyo na nguo zangu tu, vyeti vyangu vya elimu vilipona kwa sababu vilikuwa kazini,

"Inauma! Nilizungukwa, niliponea chupuchupu, nimezungukwa na risasi nyuma yangu, nikajitahidi nifike nyumbani nikakuta hakuna mtu,

"Tukatembea sana, nikafika Kigoma eneo la Kagongo, tulikuwa zaidi ya wakimbizi 5000. Mimi ndio nilikuwa kiongozi wa hao wakimbizi wenzangu," anasimulia.

Anasema katika mwambao wote wa Ziwa Tanganyika, kila sehemu walijaa wakimbizi na baada ya hapo, wakaanza kuwaona viongozi wa serikali, wakiwamo wa tarafa ya Mwandiga na anamkumbuka Mwenyekiti wa Kagongo, alikuwa anaitwa Mzee Mbombo.

Ebengo anasema, watu hao waliwapa moyo na miongozo ya kujihifadhi, ndipo baadaye walifika wafanyakazi wa Umoja wa Mataifa, waliokwishaandaa kambi ya kwanza katika eneo la Kibirizi, Kigoma.

Anasema, waliendelea kuongezeka na pakafunguliwa kambi mpya mjini Kigoma katika uwanja wa mpira Lake Tanganyika na nyingine, Maweni.

Baada ya kuongezeka, ikafunguliwa kambi ya Nyarugusu, na wote waliofikia huko, walipewa hadhi rasmi ya ukimbizi na wenzao mbao hawakupenda hadhi hiyo, waliishi katika mwambao wa Ziwa Tanganyika.

"Kurudi nyumbani kila mmoja anatamani na kutarajia kukiwa shwari. Kila mtu anatamamni kurudi katika ardhi mama. Wakati unakwenda nchi nyingine, unakuwa na woga, hofu, watanichukuliaje, je ni mhalifu?" Anasema Ebengo.

### HAKI ZA BINADAMU

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Diginity Kwanza, Janemary Ruhundwa, anashauri kuandikwe kitabu cha historia ya ukimbizi nchini, kwa miaka 60 iliyopita.

Janemary anasema, kitendo cha nchi kupokea na kuhifadhi wakimbizi, kunakopaswa kuwekwa kwenye maandishi sahihi, kwa manufaa ya utafiti na vizazi vijavyo.

"Kitabu hiki kitaandikwa na sisi Watanzania wenyewe, hivyo tumeamua kukutana na Watanzania wote ambao watakuwa na taarifa kuhusu wakimbizi," anasema Janemary, akifafanua wanalenga kuainisha mengi yaliyofanywa na serikali.

### WANASHERIA WACHAMBUA

Ofisa Hifadhi na Sheria kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani, Asnath Barnabas, anasema mwaka 1998 ilitungwa Sheria ya Wakimbizi, ikielezea wanavyoweza kuomba hifadhi na eneo la kupata huduma.

"Kuna baaadhi ya haki ambazo wanapata. Pia, wana wajibu wakiingia nchini wanakuwa waomba hifadhi," anasema.

Asnath anagusaa sheria iliyochukua baadhi ya taratibu za mkataba wa kimataifa kuhusu wakimbizi wa mwaka 1951 na iliyokuwa Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU).

Mwanazuoni wa Shule Kuu ya Sheria ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Profesa Khoti Kamanga, anasema upatikanaji taarifa kuhusu wakimbizi nchini ni mdogo, ikilinganishwa na hatua za Tanzania kuhifadhi wakimbizi kwa miaka 60 hivi sasa.

Profesa Kamanga, bingwa wa sheria za kimataifa na mshiriki wa Kituo cha Masuala ya Wakimbizi (Centre for the Study of Forced Migration) katika shule hiyo, anasema kuna kasoro katika taarifa zilizoandaliwa kuhusu wakimbizi wa Afrika, kwamba zinatoka ya nje.

"Taarifa kuhusu wakimbizi ambao kwa idadi kubwa Tanzania huwapokea zaidi tangu miaka ya 1950 hazijaandaliwa. Hii inatokana na uwekezaji mdogo, uchumi mdogo na uhaba wa wahadhiri wa kufanya hivyo.



John Ebengo, mkimbizi wa mfano kutoka DRC.



Mtaalamu wa masuala ya wakimbizi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Profesa Khoti Kamanga.

"Kunahitajika angalau Dola 500 (1,150,000) kufanya utafiti, kufika maeneo ya wakimbizi na muda wa kuandaa na kuweka kwenye maandishi. Vitabu hivi sasa tunategemea utafiti uliofanywa na nchi za nje, utafiti ambao hatuna miliki nao," anasema Profesa Kamanga.

Anasisitiza muhimu ya kuwapo kumbukumbu katika machapisho si kuishia vitabu pekee, anaendelea: "Magazeti pia ni kumbukumbu nzuri na rahisi, itasaidia kutumiwa kama nchi na kujivunia tulichokiandika wenyewe cha kwetu."

"Mfumuko wa wakimbizi ulianza miaka ya 1940, baada ya vita kuu ya kwanza ya dunia na ya pili, ila hakuna kumbukumbu. Wazee wetu wa hapa nchini wapo baadhi wana kumbukumbu hizi kichwani wanatembea nazo," anasema Profesa Kamanga.

### WANAOHANGAIKA DUNIANI

Kamishna Mkuu wa UNHCR, Filippo Grandi, anasema takriban watu milioni 80 duniani kote wamelazimika kuyahama makazi yao, kutokana na machafuko na vita.

Anaeleza rekodi yao inaonyesha, mataifa ya Syria na DRC ni miongoni mwa penye idadi kubwa ya waliokimbia makwao kutokana na machafuko.

"Idadi hiyo ni zaidi ya asilimia moja ya jumla ya watu duniani ambao ni wakimbizi, wakimbizi wa ndani na wahamiaji," anasema Grandi.

Anaeleza kuwapo udhaifu katika kushughulikia mizozo duniani na anafafanua: "Shirika la UNHCR limetoa ripoti kuhusu hali ya wakimbizi ya mwaka 2019 na kwa bahati mbaya kwa mara nyingine tena, idadi ya wakimbizi inaendelea kuongezeka kila mwaka toka mwaka 2012."

Grandi anasema, kasi ya machafuko ndio chanzo cha umma kuyahama makazi yao na ripoti ya UNHCR, inaeleza mwaka jana waliongezeka wakimbizi wa ndani na wahamiaji milioni tisa, huku kasi ya ongezeko ikiwa juu duniani kwa miaka 10 iliyopita.

AFYA

## KITUO KIPYA HOSPITALI MKOA...

# Operesheni ya lishe bora kutokomeza udumavu wa watoto mkoa Shinyanga

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

BAADA ya kilio cha yanayojiri mkoani hapa katika eneo la afya ya watoto mkoani Shinyanga, serikali kwa kishirikiana na wadau imeinuka na kuichukua hatua mara moja.

Hiyo inatokana na kuzindua kitengo cha kutoa huduma za lishe katika Hospitali ya Rufani Mkoa Shinyanga, ili kutokomeza tatizo la udumavu kwa watoto.

Ni hali inayoelezwa kusukumwa na uhalisia wa Mkoa wa Shinyanga, kuwa miongoni mwa maeneo yanayokabiliwa na tatizo kubwa la udumavu dhidi ya watoto, ikitajwa katika kiwango cha asilimia 32, huku kitaifa inabaki kuwa asilimia 34.4.

Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma za Lishe kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee, na Watoto, Grace Moshi, anasema udumavu kwa watoto wa Shinyanga, unasababishwa na ukosefu wa elimu lishe kwa wazazi, hasa waishio vijijini.

Grace anasema, serikali kwa kushirikiana na asasi ya World Vision inayotekeleza miradi ya lishe kwenye wilaya 36 nchini, zikiwamo Shinyanga, iliona uhalisia huo kuzindua kitengo cha kutoa huduma za lishe katika Hospitali ya Rufani mkoa wa Shinyanga.

Anasema, kitengo hicho kitakuwa kinatoa elimu kwa wazazi kuhusu namna ya kuzingatia lishe bora kwa watoto, tangu kutungwa mimba, umuhimu wa kunyonyesha maziwa ya mama peke ndani ya miezi sita, pamoja na kumpatia chakula bora mtoto katika ukuaji wake wote.

"Hapa ni kituo tu, bali tunataka elimu hii itolewa kwenye maeneo yote ya huduma za afya mkoani hapa, pamoja na kwenye kliniki za afya ya uzazi, ili tatizo la udumavu lipungue," anasema Moshi.

"Matatizo haya ya udumavu dhidi ya watoto wadogo huliathiri sana taifa katika sekta mbalimbali, zikiwamo za afya, elimu, pamoja na kiuchumi, wakati tatizo hili linazuilika kabisa endapo wazazi wakazingatia ushauri wa wataalamu wa masuala ya lishe bora," anaeleza.

**VIONGOZI MKOA**

Katibu Tawala wa Mkoa wa Shinyanga, Albert Msovela, anasema kitengo kitasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza tatizo la udumavu dhidi ya watoto wadogo, wazazi wakiwa na mahali sahihi pa kuwapo elimu ya lishe.

Anasema, licha ya hospitali hiyo ya rufani mkoani Shinyanga kuzindua kitengo hicho cha huduma za lishe, pia watashusha maagizo kwa mamlaka za serikali za mitaa, ili elimu itolewa hadi kwenye ngazi za wilaya, ikishuka chini waliko wananchi ikiwamo ngazi ya vijijini.

"Mtoto anapozaliwa na afya duni hata ukuaji wake una kuwa dhaifu na hawezi kuwa mzuri pia kimasomo, tofauti na yule ambaye hana udumavu," anasema Msovela.

"Ndio maana nasisitiza elimu hii ya lishe ifikie hadi maeneo ya vijijini kwa wakulima, sababu wana vyakula vingi lakini hawajui kipi ni chakula bora kwa mtoto.

"Nawaombeni sana wataalamu wa lishe msiishie tu kutoa elimu maeneo ya mjini, tembeleeni na wananchi huko vijijini, pamoja na kuwapatia elimu ya lishe kwa vitendo kama mnavyoonyesha hapa kwenye uzinduzi," anaendelea:

Ofisa Lishe Mkoa wa Shinyanga, Dennis Madeleke, anataja takwimu za udumavu kwa watoto wa Shinynga ni asilimia 32, sababu kuu ni wazazi kuwa na elimu duni ya lishe, huku serikali mkoa ikichukua hatua ya kuwapa wazazi maarifa na ujuzi kuhusu lishe bora kwa watoto.

Ni hatua inayochukuliwa kwa ushirika na mashirika mbalimbali wakitoa chanjo ya matone ya vitamini 'A' na minyoo kwa watoto walio na umri chini ya miaka mitano, pia kuwapatia tiba wenye matatizo ya udumavu.



Ofisa Lishe wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Saidi Mankiligo, akitoa maelezo kwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Shinyanga, Albert Msovela, namna ya kuzingatia mlo kamili.

**WADAU WENZA**

Mkurugenzi wa Miradi wa World Vision, Nesserian Mollel, anasema wana miradi inayohusu lishe katika katika wilaya 36 nchini, lengo ni kuhakikisha udumavu kwa watoto unakwisha, nyenzo yao kuu ya kampeni ni elimu kwa wazazi na walezi.

Pia, anasema katika utoaji elimu hiyo, wamekuwa wakikumbana na changamoto kwa jamii wanaoshindwa kutoa kipaumbele na kutotambua makundi ya chakula bora, hasa maeneo ya vijijini ambako katika uhalisia kuna utajiri wa vyakula.

"Tunatekeleza mradi huu wa lishe (ENRICH) takribani miaka mitano sasa. Bado jamii inahitaji kupewa elimu ya lishe zaidi, licha ya kuwapo na mafanikio kwa baadhi ya wazazi ambao wameshapatia elimu hii na sisi tutaendelea kushirikiana na serikali hadi kulimaliza kabisa tatizo," anasema Mollel.

**MKAZI ASIMULIA**

Dina Ibrahimu, ni mkazi wa kijiji cha Wishiteleja wilayani Kishapu, mkoani Shinyanga, eneo ambalo World Vision wanatekeleza mradi wa lishe, anatoa ushuhuda binfasi wa kujifungua mtoto aliyekuwa na udumavu, kutokana na uelewa duni, lakini baada ya kupewa elimu hiyo mtoto wake sasa ana afya njema.

Anasema, wanawake wengi wa vijijni bado hawana uelewa na wanaishi kwa kufuata mila na utamaduni wa kizamani wakiwapatia watoto chakula bila ya kujali makundi bora ya chakula na ndio maana wanapata udumavu na kiribatumbo.

"Ninachoomba elimu hii ya lishe iendelee kutolewa zaidi hasa maeneo ya vijijini. Bado wanawake wengi hawana uelewa kabisa wa masuala haya ya lishe, yaani watoto wanapewa tu vyakula sawa na watu wazima, sababu ni kwamba hawajui ni vyakula gani wanapaswa kupewa kulingana na umri wao," anaongeza Ibrahimu.




Mzazi Dina Ibrahimu mkazi wa kijiji cha Wisheteleja wilayani Kishapu, akitoa ushuhuda namna elimu ya lishe bora ilivyookoa afya ya mtoto wake, aliyezaliwa akiwa na uzito pungufu. **PICHA ZOTE: MARCO MADUHU**





Msukuma toroli akipita kwa tahadhari huku akiwa amebeba mzigo kwenye barabara iliyojaa maji pembezoni mwa soko la Sabasaba jijini Dodoma, kutokana na mvua kubwa iliyonyesha jana na kusababisha madereva wa maroli na mkokoteni wanaotumia barabara hiyo kushindwa kupita. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Kanisa lampongeza JPM tamko la mali

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

KANISA la Makedonia Missions Centre chini ya Calvary Assemblies of God Kisasa jijini Dodoma, limempongeza Rais John Magufuli, kwa hatua yake la kuwataka watumishi wa umma kujaza fomu za matamko ya rasilimali na madeni kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi Namba 13 ya mwaka 1995.

Mbali na pongezi hizo, kanisa hilo limewataka watumishi wa umma ambao baadhi yao wapo makanisani na misikitini, kutotumia nafasi zao kujificha katika vivuli vya sehemu zao za ibada.

Pongezi hizo zilitolewa jana na mwasisi wa kanisa hilo, Mchungaji Vicent Malenda, alipokuwa akizungumza na vyombo vya habari jijini hapa, ikiwa ni sehemu ya salamu zake za maandalizi ya kumaliza mwaka 2020 na kuukaribisha mwaka 2021.

Malenda alisema kitendo cha watumishi wa umma kusisitizwa kujaza fomu za maadili kitajenga heshima kwa kuwa kila mmoja atakuwa na nidhamu ya kazi aliyo nayo. "Suala la kujaza fomu si jambo geni, lakini lilikuwa kama limesahaulika na kusababisha baadhi ya watumishi wa umma kujisahau na hatua hiyo ilisababisha watu kujipatia mali kwa njia ya ujanja ujanja. "Lakini wapo baadhi ya watumishi wa umma ambao wapo kwenye maeneo mbalimbali ya nyumba za ibada wamekuwa wakitumia nafasi zao kuwakandamiza watu ambao wanadai haki zao na hasa wanapokuwa karibu na viongozi wakuu wa dini husika," alisema.

Kiongozi huyo wa kiroho alisema mtumishi wa umma ni lazima akaonyesha maadili yake awapo kazini au nje ya kazi na kuwa kielelezo na mpatanishi kati ya jamii na viongozi wa dini pale inapotokea mgogoro.

Pia alisema wako baadhi ya viongozi wakuu wa dini ambao wanawatumia waumini wao wenye mamlaka serikalini kuwanyanyasa baadhi ya waumini ambao wanaonekana kudai haki zao kunapokuwapo na mgogoro.

"Unaweza kushangaa labda katika kanisa au mahali popote kunatokea mgogoro labda ya kimadai na mmoja anaamua kwenda katika vyombo vya sheria, lakini kwa kuwa ndani ya kanisa kuna kiongozi mkubwa serikalini, uamuzi unachukua muda mrefu.

"Naomba kutoa rai kwa viongozi wa dini kutowatumia vibaya waumini ambao wananafasi kubwa katika utumishi wa umma katika kukandamiza upatikanaji wa haki bali wasimamiwe kuhakikisha wanatunza maadili ya kazi yao pindi wawapo kazini au nje ya kazi," alisisitiza Malenda.

Kuhusu elimu, kiongozi huyo aliwataka wazazi na walezi kuhakikisha wanaandaa mazingira bora na wezeshi ya kuwapeleka shule watoto wenye sifa.

# Bahi yajizatiti kuongeza ufaulu 2021

**Na Paul Mabeja, BAHI**

HALMASHAURI ya Wilaya ya Bahi mkoani Dodoma imeweka mikakati ya kuboresha elimu na kuongeza ufaulu kwa wanafunzi wa sekondari na shule za msingi katika mwaka wa masomo 2021.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Donald Mejeti, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mikakati ya wilaya hiyo kuboresha elimu na kuongeza ufaulu mwakani.

Alisema pamoja na wilaya kushika nafasi ya kwanza katika ufaulu kwa wanafunzi wa darasa la saba kimkoa mwaka huu, bado kuna haja ya kuongeza juhudi zaidi, ili kupandisha ufaulu.

"Juzi tulifanya kikao kilichojumuisha wakuu wa shule za msingi na sekondari, waratibu elimu kata, wadhibiti ubora elimu, Chama cha Walimu (CWT), Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri na Mkuu wa Wilaya, kikao ambacho nilikiitisha lengo likiwa kuboresha elimu na kuweka mikakati ya kuongeza ufaulu mwakani," alisema Mejeti.

Alisema baada ya kikao hicho, kikao kingine kitawajumuisha watendaji wa kata na vijiji, ili kusaidia kuhamasisha wananchi kutambua mchango wao katika kuboresha elimu katika wilaya hiyo.

"Tunataka wananchi watambue umuhimu wao katika kujitolea nguvu kazi kwenye ujenzi wa vyumba vya madarasa pamoja na samani kwa maana ya madawati pamoja na vifaa vingine vinavyohitajika katika sekta ya elimu," alisema Mejeti.

Alisema, halmashauri hiyo inaupungufu wa vyumba vya madarasa 11, ambavyo vinahitaji ile kuwezesha wanafunzi waliokosa nafasi kuanza masomo kama serikali ilivyoagiza.

"Kutokana na kikao tulichokaa tunaamni hivi vyumba vya madarasa 11 hadi Januari 30, mwakani, tutakuwa tumekamilisha ujenzi wake na watoto kujiunga na masomo yao kama ambavyo imeelekezwa na serikali ifikapo Februari 28, alisema.

Pia alisema lengo la wilaya hilo ni kuhahakikisha inafanya vizuri katika sekta ya elimu kimkoa na kitaifa katika ufaulu wa shule za msingi na sekondari tofauti na ilivyo sasa.

# Wanufaika msaada wa vifaa vya elimu

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

ZAIDI ya wanafunzi 100 kutoka familia maskini nchini kuendelea kunufaika na msaada wa vifaa vya elimu kutoka Taasisi ya Dk. Ombeni Msuya.

Mkurungenzi wa Taasisi hiyo na Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Dk. Ombeni Msuya, alibainisha hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa.

Dk. Msuya alisema zaidi ya wanafunzi 100 kutoka maeneo mbalimbali nchini wananufaika na vifaa vya elimu kupitia taasisi hiyo.

"Kimsingi taasisi yetu inasaidia watoto wengi maeneo mbalimbali nchini, lakini hawa tuliowataja ni wale ambao tumekuwa nao kwa kipindi cha zaidi ya miaka mitano iliyopita," alisema.

Pia alisema taasisi hiyo inawasaidia wanafunzi hao vifaa vya elimu kama madaftari, sare za shule, kalamu na mahitaji mengine kwa ajili ya kujikimu.

Hata hivyo, alisema kuna wanafunzi wengine zaidi wananufaika kupitia misaada ya vifaa hivyo inayotolewa na taasisi kwenye baadhi ya shule nchini.

Alisema utaratibu wa kuwatambua walengwa wa misaada hiyo umekuwa ukifanywa na uongozi wa shule husika au halmashauri.

Kadhalika, Dk. Msuya alisema kuna wanafunzi 21 wamemaliza kidato cha sita na wengine 45 wanaendelea na masomo ya kidato cha tano na sita katika shule mbalimbali nchini.

Alitaja mikoa ambayo walengwa hao wanapatiwa misaada na taasisi hiyo kuwa ni Morogoro, Iringa, Lindi, Kilimanjaro, Mtwara, Pwani na Dodoma.

Aliongeza kuwa taasisi hiyo ilisaidia kutengeneza meza 67 na viti 45 katika Shule ya Sekondari ya Ibihwa wilayani Bahi na madawati 20 katika Shule ya Sekondari ya Sechelela jijini hapa.

Sambamba na hayo, Dk. Msuya alisema taasisi inalenga kutoa mashine za kurudufu (photocopy machines) kwa shule za sekondari za Mpwapwa iliyopo Wilaya ya Mpwapwa na Ibihwa.

Alisema lengo la taasisi hiyo ni kuendelea kusaidia serikali katika kuihudumia jamii kwenye sekta ya elimu, maji na kujenga miundombinu msingi.






Mmoja wa wanufaika wa bima ya afya iliyoboreshwa ya CHF katika Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, mkoani Mbeya, akipokea kadi yake ambazo zimetokana na michango ya kikundi cha Ibhasa Festival, kusaidia waishio kwenye mazingira magumu, jumla ya wananchi 662 wamenufaika. **PICHA GRACE MWAKALINGA**

## Mazingira magumu wasaidiwa matibabu

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

ZAIDI ya Sh. milioni tatu zimetumika kuwakatia bima ya afya wananchi 662 wanaotoka kwenye mazingira magumu katika wilaya ya Kyela mkoani Mbeya kupitia Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) iliyoboreshwa.

Kutokana na msaada huo, wananchi hao watapata huduma za afya bure kuanzia ngazi ya zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya hadi za rufani za mikoa na kanda.

Msaada huo ulitolewa na kikundi cha Ibhasa Festival 2020 kwa kuchangia fedha taslimu, ili kuwawezesha watu hao kupata huduma za afya.

Michango hiyo ilitokana na wazawa wa Kyela waishio maeneo mbalimbali ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuwasaidia wananchi wenye mahitaji hususani kwenye sekta ya afya na Makamu Mwenyekiti wa Ibhasa Festival 2020, Edo Mwamalala, alisema kikundi hicho kimekuwa na mchango mkubwa katika kuisaidia jamii ya Kyela katika sekta za afya na elimu kwa miaka miwili mfululizo.

Alisema kwa mwaka huu waliamua kujikita kusaidia matibabu kupitia bima ya afya iliyoboreshwa kwa makundi yenye mahitaji maalum.

Mjumbe wa Kamati ya Ibhasa Festival 2020, Nicolaus Mwangomo, alisema moja ya mikakati yao ni kuboresha zaidi sekta za afya na elimu kwa kuhakikisha wanayafikia maeneo yote ya Kyela ambayo yana uhitaji na kuwaomba wadau wengine kuchangia mpango wa CHF ili kuwahakikishia wananchi upatikanaji wa huduma za afya.

Mwangomo aliiomba serikali kuboresha mazingira ya kutolea huduma kupitia dirisha la CHF kama inavyofanya kwa makundi mengine ya bima ya Afya na kwamba ni vyema CHF ikawekewa umuhimu ili wananchi wapate huduma za matibabu bila vikwazo vyovyote.

"Moja ya mikakati ya serikali ni kuhamasisha wananchi kujiunga na mifuko ya bima ya afya lengo likiwa ni kuboresha huduma za afya kupitia michango hiyo. Kikubwa ni dirisha la CHF kuboreshwa kwa sababu kuna malalamiko baadhi ya wananchi wanasema utoaji huduma hauridhishi," alisema Mwangomo.

# RC atangazia kiama wakwepa kodi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI mkoani Mbeya imetangaza kuanza kuwasaka wafanyabiashara wanaokwepa kodi kwa kuchezea mashine za kielektroniki za kutolea risiti (EFD) na kuwachukulia hatua kali za kisheria.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alisema ameiagiza Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kuanza msako huo ikiwa ni pamoja na wale ambao wanauza bidhaa bila kutoa risiti licha ya kuwa na mashine hizo.

Chalamila alisema wafanyabiashara ambao watakamatwa watafikishwa mahakamani na kufunguliwa mashtaka pamoja na kufungiwa biashara zao ili iwe fundisho kwa wengine ambao wana tabia za aina hiyo.

Alisema lengo la serikali ni kukusanya kodi ili kupata fedha za kuendeshea miradi mbalimbali ya maendeleo na kuwa na uwezo wa kujitegemea kibajeti.

"Tumegundua wapo wafanyabiashara mkoani hapa wanakwepa kodi kwa makusudi. Wanakwepa kutoa risiti kwa wananchi wanaowahudumia. Sasa hatuwezi kukubali ni lazima hatua zichukuliwe dhidi yao kuanzia sasa," alisema Chalamila.

Alisema moja ya kesi zitakazowakabili wafanyabiashara watakaokamatwa kwa kosa hilo ni pamoja na kesi za uhujumu uchumi ambao ni mbaya kutokana na kutokuwa na dhamana.

Mkuu wa Mkoa aliwataka wafanyabiashara kuacha tabia hiyo mara moja kwa kuwa madhara yake ni makubwa endapo watabainika na kwamba serikali haipendi kukimbizana na wananchi wake, lakini wafanyabiashara hao wanajaribu kuilazimisha.

"Lakini hata wananchi ambao wananunua bidhaa za fedha nyingi bila kudai risiti wajue kwamba wanachokifanya ni kosa, hivyo na wao mkono wa sheria utawahusu. Nawatahadharisha sana wawe makini," alisema.

Baadhi ya wananchi waliiomba serikali kuendelea kuta elimu ya ulipaji kodi kwa maelezo kuwa wengine hawana ujuzi na hawajui faida ya kulipa kodi na hata namna ya kulipa kodi hawajui.

Mmoja wa wananchi hao, Israel Mswelo, alisema baadhi ya wafanyabiashara wamekuwa wakiwauzia bidhaa, lakini wakiwadai risiti wanagoma wakidai kuwa mashine za kutolea risiti zimeharibika.

Alisema wako pia baadhi ya wananchi ambao wananunua vitu, lakini hawajui umuhimu wa kudai risiti na hivyo huwa wananunua bidhaa na kuondoka bila kupewa risiti.

# Matumaini wananchi kupata maji yafufuka

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

MATUMAINI ya wananchi wa vijiji 16 vya Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya kupata maji ya bomba, yamefufuka baada ya serikali kutoa zaidi ya Sh. bilioni 2.3 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa mradi wa Bwawa la Matwiga ambao ulikwama kwa takriban miaka 16.

Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi, juzi alifanya ziara ya kukagua ujenzi wa mradi huo kuanzia kwenye bwawa, tangi la kuhifadhia maji, mitaro iliyochimbwa kwa ajili ya kupeleka maji kwa wananchi na kituo cha kuhifadhia mabomba.

Baada ya kufanya ukaguzi huo, Naibu Waziri alieleza kuridhishwa na utekelezaji wake na kuwapongeza watendaji wa Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA) kwa kusimamia vizuri ukamilishaji wa mradi huo ambao sasa unaonyesha mwelekeo.

Alisema awali mradi huo ulikuwa haukamiliki kutokana na utendaji mbovu wa baadhi ya waliokuwa watendaji wa serikali ambao kwa sasa walishaondolewa na kuletwa wapya ambao wanafanya kazi vizuri.

Mhandisi Mahundi alisema analifahamu vizuri bwawa hilo kwa sababu kabla hajaenda kugombea ubunge, alikuwa Mkuu wa Wilaya ya Chunya kwa zaidi ya miaka miwili.

"Lengo la serikali ni kuhakikisha kinamama wa vijiji hivi 16 wanaondokana na kero hii ya kujitwisha ndoo kichwani tatizo ambalo ni la kihistoria. Mradi unaridhisha na nimeona vifaa vyote vimeshafika kwa hiyo naamini kufikia Machi, mwakani, wananchi wataanza kunywa maji ya bomba," alisema Mahundi.

Akitoa taarifa ya ujenzi wa mradi huo, Meneja wa RUWASA Wilaya ya Chunya, Mhandisi Ismail Nassor, alisema mradi huo unatekelezwa kwa kutumia akaunti ya dharura (Force account) ambayo inatumia mafundi wa mitaani.

Alisema kwa mujibu wa mkataba, mradi huo unatarajiwa kukamilika Machi 30, mwakani, na kwamba utaanza kuvinufaisha vijiji viwili vya awali ambavyo ni Matwiga na Isangawana ambavyo viko jirani zaidi na mradi.

Ujenzi wa bwawa, alisema ulishakamilika na sasa kinachofanyika ni ujenzi wa miundombinu ya kusambaza maji kutoka kwenye bwawa kupeleka kwa wananchi. "Tumejenga tangi lenye ujazo wa lita 500,000 ambalo liko katika hatua za mwisho, tumechimba mitaro na kulaza mabomba ya kupeleka maji kwa wananchi kilomita 26 na kuanzia wiki ijayo tunaanza kujenga vituo 36 vya wananchi kuchotea maji," alisema Nassor.

Baadhi ya wananchi wa Kata ya Matwiga walisema walikuwa wameshakata tamaa ya kupata maji kutoka kwenye bwawa hilo, lakini kwa sasa matumaini hayo yamefufuka na wanashiriki kwenye shughuli za ujenzi.

Mmoja wa wananchi hao, Atupyelesyeghe Mtawa ambaye ni Mwenyekiti mstaafu wa Kijiji cha Matwiga, alisema kwa muda mrefu wananchi wa maeneo hayo wamekuwa wakihangaika kwa muda mrefu kupata maji ya kunywa.

Alisema mradi wa maji wa Matwiga ulipopelekwa na serikali, walianza kupata matumaini ya kuanza kunywa maji ya bomba, lakini kutokana na kusuasua kwa muda mrefu walikata tamaa.



# Jamii yatakiwa kuzingatia mazoezi ya mwili

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MENEJA wa Kitengo cha Maradhi yasiyoambukiza kutoka Wizara ya Afya Zanzibar, Omar Ali Abdalla, ameitaka jamii kuwa na utamaduni wa kufanya mazoezi ili kuepuka visababishi vya maradhi yasioambukiza.

Akizungumza na waandishi wa habari katika Ofisi ya Jumuiya ya watu wanaoishi na maradhi yasioambukiza Zanzibar iliyopo Mpendae, alisema janga la maradhi hayo linatokana na vichocheo mbalimbali ikiwamo kukosekana mlo kamili na kutofanya mazoezi.

Alisema kuwa ipo haja wananchi kufanya mazoezi angalau kwa dakika 30 kwa siku, ili kupunguza uzito jambo ambalo litasaidia kuondoa vichocheo vya maradhi yasioambukiza ikiwamo shinikizo la damu, kisukari na msongo wa mawazo. "Kinga ni bora kuliko tiba, ukipata maradhi yasiyoambukiza si rahisi kupoa bali utapewa ushauri nasaha wa utaratibu wa kuishi," alisema Meneja Omar.

Alisema imebainika kuwa wananchi wengi wa Zanzibar wanashiriki kufanya mazoezi, lakini wengi wao hawafikii malengo na wengine hawafanyi kabisa.

Hata hivyo, alisema kwa wenye matatizo wakiwamo wajawazito na watu wanaoishi na maradhi yasiyoambukiza ni vyema wakafuata ushauri wa daktari.

Alisema si lazima kufanya mazoezi ya kukimbia, lakini hata kutembea kwa mwendo wa haraka kunasaidia.

Pia aliwataka wazazi na walimu wa michezo kuhamasisha wanafunzi kufanya mazoezi shuleni ili kuwa wachangamfu kimwili na kiakili.

Alisema mazoezi husaidia kujenga mwili na kukua kiakili na kuondoa maradhi mbalimbali ikiwamo yasiyoambukiza na msongo wa mawazo.

Akizitaja changamoto zinazojitokeza katika kufanya mazoezi alisema kuwa ni pamoja na ukosefu wa elimu sahihi ya ufanyaji wa mazoezi, hasa kwa watu wenye ulemavu.

Aliiomba idara ya mipango miji kuendelea kuzilinda sehemu za wazi ili jamii itumie kwa mazoezi.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, akiwa katika ziara ya ghafla pembezoni mwa chemuchem ya Mto Pepo iliyopo bomba kuu la kusafirisha maji ambalo linavuja kwa zaidi ya wiki mbili sasa. **PICHA: OMPR**

# ZAWA yaagizwa kutengeneza bomba linalovuja

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

UONGOZI wa Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) kwa kushirikiana na Wizara ya Maji na Nishati, umetakiwa kulifanyia marekebisho ya haraka bomba kuu la kusafirisha majisafi na salama pembezoni mwa chemchem ya Mto Pepo, mjini Unguja, linalovuja kwa wiki tatu sasa ili kunusuru rasilimali hiyo muhimu.

Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, alitoa agizo hilo alipofanya ziara ya ghafla katika eneo hilo baada ya kupata taarifa kutoka kwa wananchi kuhusu umwagikaji ovyo wa maji.

Akitoa agizo hilo alisema wapo baadhi ya wananchi katika maeneo mbalimbali bado wanaendelea kukosa huduma hiyo wakati baadhi ya sehemu inaendelea kumwagika bila ya kuchukuliwa hatua za dharura.

Alisema maji yanayopotea katika eneo hilo lazima viongozi hao wanaohusika na usimamizi wa huduma hiyo waandae utaratibu utakaohakikisha unalitafutia suluhu tatizo hilo ambazo Serikali Kuu haipendelei kuliona linaendelea kuwapo.

Alimwagiza Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Maji Zanzibar kumpangia kazi nyingine Mhandisi Mtendaji wa mamlaka hiyo aliyepewa jukumu la kufanya ukaguzi wa kuipitia miundombinu ya maji na kushindwa kutoa ripoti ya uwapo wa tatizo hilo.

Akitoa taarifa ya bomba hilo Mkurugenzi Mkuu wa ZAWA, Mussa Ramadhan Haji, alisema bomba hilo lililojengwa mwaka 1923, likiwa limeshadumu kwa takriban miaka 97 sasa linahudumia maji yanayotoka katika chemchema ya Mtopepo na kupeleka katika tangi kuu liliopo Saateni. Mussa alisema bomba hilo lililokuwa chini ya ardhi wakati wa ujenzi limezungukwa na mmong'onyoko wa ardhi pamoja na ujenzi holela wa nyumba za makazi hali iliyochangia kuchakaa na tayari limeshaanguka zaidi ya mara mbili na kufanyiwa matengenezo makubwa.

Alisema suluhu pekee ya kukabiliana na tatizo hilo ni kuingizwa katika mradi mkubwa wa kubadilishwa kwa bomba hilo kazi ambayo endapo itafanyika wananchi watalazimika kukosa huduma za maji si chini ya wiki tatu.

Kwa upande wake Sheha wa Shehia ya Banko, Juma Bakari, alisema tatizo la uvujaji wa huduma hiyo wamelitolea taarifa kwenye mamlaka husika, lakini wahandisi wa Mamlaka ya Maji wamechukua muda mrefu kulitafutia ufumbuzi.

## ZAECA yaokoa mil. 33/- walizotapeliwa wananchi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAMLAKA ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar (ZAECA), imefanikiwa kuokoa fedha za wananchi Sh. 33,130,000.

Fedha hizo zilizookolewa ni za wananchi ambao walidhulumiwa kwa kuahidiwa kupatiwa ajira.

Akizungumza na waandishi wa habari, Naibu Mkurugenzi wa uchunguzi na operesheni wa mamlaka hayo, Makame Khamis Hassan, alisema wananchi waliodhulumiwa ni 58, ambao walitozwa fedha hizo na watu ambao sio watumishi wa umma (matapeli) na kuwaahidi kuwapatia ajira katika idara na taasisi tofauti za umma ikiwamo idara maalum za SMZ, sekta ya mafuta na gesi pamoja na sekta ya afya.

"Baada ya kupokea taarifa hii ZAECA ilifuatilia na ufanikiwa kuzipata fedha hizo kutoka kwa matapeli hao," alisema.

Alisema tayari ZAECA imewakabidhi fedha hizo vijana wote waliokumbwa na mkasa huo na kuufahamisha umma kwamba ajira za serikali haziuzwi na hakuna mtu ambaye amepewa uwezo wa kuuza ajira za serikali.

Alisema kukubali kutoa fedha kwa madhumuni ya kununua ajira nalo ni kosa la jinai (rushwa), pamoja na mahitaji yaliyopo ya ajira hivyo wananchi kutokubali kutoa fursa kwa matapeli wa aina hiyo.

Alieleza kuwa serikali imeandaa utaratibu maalum kupitia vyombo ilivyounda kushughulikia suala zima la uajiri nchini.

Aliwataka wananchi wasisite kutoa ushirikiano kwa ZAECA pale tu watakapobaini kwamba kuna udanganyifu katika kutafuta huduma za umma.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA SHULE

Keland Nursery and Primary School iliyopo Salasala Rtd inatangaza Nafasi Za Awali Na Msingi. Mawasiliano : 0713327613.


## OFISI ZA MATANGAZO

Mikocheni Industial Area,
Po.Box 31042, Dar es Salaam. Mob: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com


## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**SELEMANI MOHAMED CHAMLE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **ISUZU FORWARD** yenye namba za usajili T 934 DNV.Chassis No **FRR35L37000713,** Engine **No. 6HL1349258.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/MPW/RB/889420/2020.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Sumagro Ltd,** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA HILUX 2.4D** yenye namba za usajili **T 993 AFW,** Chassis **No.LN650062405,** Engine **No.2L 1515315,** yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi

**Polisi taarifa CONTROL NAMBA 9910820038587**

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**FRED ONISAEL SWAI** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **HAOJUE** yenye namba za usajili **MC 597 CBE.** Chassis **No. LC6PCJK22J0051782,** Engine No. **156FMI-5A*D2F42270*.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/MPW/RB/201270/2020.**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO......OF 2020**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE ANNA LUSINDE MALECELA**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMISTRATION BY MULAMU NGHAMBI**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the ...... day of ...... 2020.
Dated at Dodoma this 2nd day of December 2020
Presented for filling this 11th day of December 2020

Presented for filing this 11th day of December 2020

COURT SEAL DODOMA DISTRICT

MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE DODOMA DISTRICT

## TANGAZO KUPOTEA OFA YA KIWANJA

**KARANGI J.B. BWIRE** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA OFA YA **KIWANJA NAMBA 768 KITALU "DD"** MAJENGO MAPYA MANISPAA YA SHINYANGA. KWA YEYOTE ATAKAE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU AU AWASILIANE NA KARANGI BWIRE KWA **SIMU NAMBA 0767 500472 RB NAMBA SHY/RB/2020/ CONTROL NAMBA 9910819671611.**

MUSA J. MAKUNGU
AFISA ARDHI
**SHINYANGA.**
AFISA ARDHI WA MANISPAA SHINYANGA







UZA, CHENYE THAMANI KUBWA KWA KUTANGAZA NASI
KWA BEI POA TUPIGIE MOB: +255 - 745 700 710



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Wanafunzi 40,000 Kenya kusoma kwa redio

**Nairobi, KENYA**

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la kuhudumia Watoto (UNICEF), limegawa redio 10,000 za nishati ya sola, kwa kaya maskini nchini Kenya, ili watoto wapate fursa ya kusoma nyumbani wakati huu wakijiandaa kurejea shuleni.

Watoto 40,000 watafaidika na msaada huo wa redio za sola baada ya UNICEF kutambua athari za kufungwa shule wakati huu wa COVID-19 hasa kwa kaya maskini.

Katika eneo la mtaa wa mabanda la Kibera jijini Nairobi, mwanafunzi wa sekondari, Selina Nakesa Mamati, alisema amekosa shule kwa miezi nane iliyopita na yuko nyuma kimasomo.

Alisema atakaporejea shuleni Januari, mwakani itambidi aanze upya.

Selina ambaye ni miongoni mwa wanafunzi hao, alisema kukaa nyumbani kumemchosha na akiamka anachokifanya ni shughuli za nyumbani na ndipo asome. Mkuu wa Mawasiliano wa shirika hilo, Kenya, Andrew Brown, alisema kufungwa kwa shule kumeingilia masomo kwa mamilioni ya wanafunzi nchini humo, ambao wamekosa zaidi ya miezi sita ya masomo rasmi.

"Wote tumeisaidia serikali kwanza kwa watoto kusomea nyumbani na pili kwa maandalizi ya shule kufunguliwa kwa usalama," alisema Brown.

Mkurugenzi wa Elimu wa Kaunti, Lydia Mugeti, alisema msaada wa UNICEF, umekuwa ni nuru gizani kwa kuwa redio 100 zilizogawanywa katika mtaa huo wa mabanda, watoto zaidi wamepata fursa ya kusikiliza masomo redioni na wasio nazo kwenda kwa jirani kusikiliza.

Selina alisema redio ya sola imemsaidia kwa sababu kuna vitabu ambavyo anasoma shuleni, anavipata kupitia redio.

Ruth Mamati, alisema wanawe kusalia nyumbani bila masomo ilimwathiri.

"Janga la corona sio tu kwamba liliathiri wanangu bali na mimi pia imeniathiri, upande wa kazi hivyo sote tumesalia nyumbani.

Imenipa changamoto nyingi sana kwa sababu wanataka kula, wanataka mahitaji ya lazima ya siku wakati mwingine hayapatikani. Unajua wakiwa shuleni inanirahisishia kazi kwa sababu wanashinda huko kuna mahitaji mengine nayaepuka."

Ingawa ni shule chache zilizofunguliwa, UNICEF inasema inaendelea kusaidia wanaosomea nyumbani hadi pale shule zote zitakapofunguliwa kwa usalama.

*UN*



Vijana wa shule walioachiwa huru na watekaji, wakiwa kwenye mkutano na Rais wa Nigeria, Muhammadu Buhari, baada ya kuachiwa Desemba 18, huko Katsina, Nigeria. **PICHA/AP**

# Polisi afutwa kazi kisa mauaji Mwafrika

**Ohio, MAREKANI**

OFISA wa polisi aliyehusika na mauaji ya raia wa Marekani mwenye asili ya Kiafrika asimamishwa kazi.

Ofisa huyo amefutwa kazi katika mji wa Columbus, Jimbo la Ohio nchini Marekani.

Mkurugenzi wa Usalama wa Umma wa Columbus, Ned Pettus, alitoa taarifa kuhusu mauaji ya Andre Maurice Hill, mwenye umri wa miaka 47 na aliye na asili ya Kiafrika, yaliyotekelezwa na polisi Desemba 21.

Pettus alitangaza kwamba, ofisa wa polisi Adam Coy, ambaye alimuua Hill, alifutwa kazi kwa sababu ya utovu wa nidhamu na uzembe.

Alibainisha kwamba, Hill, alicheleweshwa kupewa huduma ya kwanza.

"Kitendo cha Hill kufyatuliwa risasi ni janga kwa jamii yetu na polisi, na kwa mtu yeyote unayempenda," alisema Pettus.

Aliongezea kuwa vitendo vya Coy, havikidhi kiapo cha polisi wala kuendana na vigezo vya polisi vya Columbus.

Coy, alisimamishwa kazi wiki iliyopita kama sehemu ya uchunguzi ulioanzishwa dhidi yake na kesi ya kiutawala ilifunguliwa dhidi ya maofisa wengine katika eneo la tukio.

Hill, ambaye alikuwa katika karakana yake ya nyumbani, alifyatuliwa risasi na polisi na kufariki papo hapo.

Kulingana na kamera ya polisi, maofisa walipofika eneo la tukio, Hill alionekana akielekea kwa maofisa wenzie na simu yake ya mkononi.

*TRT*

# Wanausalama watia shaka utekaji watoto

**Katsina, NIGERIA**

WATAALAMU wa usalama wa Nigeria, wamesema wanatilia shaka kuwa, uhasama kati ya wakulima na wafugaji wa ng'ombe umesababisha wimbi la utekaji nyara hivi karibuni katika Jimbo la Katsina, lililopo Kaskazini Magharibi mwa nchi.

Wanafunzi wa kiume zaidi ya 300 walitekwa nyara mapema mwezi huu na baadaye wakaachiliwa huru.

Mamlaka ya Katsina mwanzoni ililaumu utekaji nyara wa wavulana wa shule 344 kwa magenge ya majambazi, ambao wamewateka nyara baadhi ya watu kwa ajili ya kulipwa fidia katika jimbo la Kaskazini Magharibi mwa Nigeria.

Aidha, maofisa walibadilisha usemi wao, wakidai utekaji huo unahusiana na mzozo kati ya wafugaji ng'ombe na wakulima kutokana na matumizi ya ardhi.

Kamishna mstaafu wa Polisi na Mchambuzi wa Usalama, Lawrence Alobi, alisema hakubaliani na madai hayo, kwamba wafugaji walifanya shambulizi hilo.

"Wafugaji hawana shida yoyote na wakuu wa shule au wanafunzi. Shida yao iko kwa wakulima, mahali ambako wanaweza kulisha ng'ombe wao. Kwa hivyo, sijui uhusiano kati ya utekaji nyara wa wanafunzi hao na mivutano na wakulima," alisema Alobi.

Kikundi cha wanamgambo wa Kiislam Boko Haram kilidai kuhusika na utekaji nyara wa wavulana hao wa shule na kutoa picha ya video inayoonyesha baadhi ya wavulana waliotekwa kabla ya kuachiliwa huru.

Madai hayo, ikiwa yatathibitishwa, yangeashiria mabadiliko kwa kundi hilo, ambalo hadi sasa limekuwa likifanya kazi hasa katika upande wa Kaskazini Mashariki mwa nchi.

Mtaalamu wa Usalama, Kabir Adamu, alisema anaamini utekaji nyara huo, ulitekelezwa na majambazi walifanya hivyo kwa maagizo kutoka kwa kiongozi wa kundi la Boko Haram, Abubakar Shekau.

"Wito utakuwa umetolewa nae. Kilicho cha muhimu zaidi ni nani anayetoa maagizo. Kwa hivyo, ikiwa vikundi vya majambazi waliofanya mashambulizi wamejiweka chini ya mamlaka ya Shekau, basi inamaanisha ndiye yeye ambaye hatimaye aliyetoa maagizo," alisema Kabir.

Mizozo kati ya wafugaji ng'ombe na wakulima wa mazao imekuwapo nchini Nigeria kwa miaka mingi, na maelfu ya watu waliuawa wakati wa mapigano makali ya ardhi kwa ajili ya malisho.

Chama cha wafugaji wa ng'ombe cha Miyetti Allah, hakikuzungumza juu ya shutuma kutoka kwa polisi, lakini kikundi hicho kilishiriki katika kujadili kuachiliwa kwa wavulana wa shule.

Alobi alisema kulaumu mapigano ya wakulima na wafugaji kwa utekaji nyara kunaweza kutupilia mbali uwezekano wa kupanua msimamo mkali katika maeneo mengine ya nchi.

"Serikali inajaribu kutumia saikolojia ya watu ili kuwaondoa hofu, lakini nadhani serikali inapaswa kuwa ya kweli kwa watu ili kila kitu kitekelezwe kufuatana na hali halisi," alisema Alobi.

Mamlaka nchini Nigeria, mwaka 2016 ilitangaza kwamba kundi la Boko Haram, limeshindwa na hivi karibuni lilikanusha madai ya kundi hilo juu ya utekaji nyara.

*VOA*

HABARI MICHEZO



# LUKAKU

## AJIWEKA NDANI YA 5-BORA YA MASTRAIKA

**MILAN, Italia**

NYOTA wa Inter Milan, Romelu Lukaku amesema anajiona kuwa "ni mmoja wa washambuliaji watano bora duniani kwa sasa" katika kuelezea namna makocha walivyombadilisha kimtazamo.

Straika huyo alizungumza na waandishi wa habari katika jarida la michezo la Voetbal Magazine la Ubelgiji juu ya soka lake la kulipwa na mafanikio ya sasa kule Italia.

Lukaku ambaye anasisitiza kuwa kila anapoingia uwanjani lengo lake huwa moja tu, ushindi, anaamini mtazamo wake huu ni muhimu zaidi nchini Italia, na ni sehemu ya mafanikio yake.

Staa huyu wa zamani wa Manchester United amebainisha kuwa kuna tofauti kubwa sana ya soka la Italia na Uingereza, na Italia anafanya zaidi kile wanachomhitaji afanye, ndicho anachozingatia na kwa namna yoyote hataki kutengeneza mazingira ya kumkwamisha juu ya hilo.

"Kwa miezi mitano iliyopita, najiweka katika orodha ya washambuliaji watano bora duniani kwa sasa. Sitaki kuandaa orodha ya wengine, lakini najiona niko ndani," alisema Lukaku.

Nyota huyu alisema makocha wamembadilisha sana kimtazamo na namna anavyoliona soka, na vile anavyofanya kazi.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, amecheka na nyavu mara 15 katika mechi 18 katika mashindano yote msimu huu, pamoja na kutoa pasi mbili za mwisho.

# ARTETA SASA AANZA KUTAMBA ARSENAL

**LONDON, England**

ARSENAL sasa ipo kwenye "dunia tofauti", kwa mujibu wa kocha, Mikel Arteta, baada ya kupata ushindi mfululizo wa Ligi Kuu England kwa mara ya kwanza tangu Septemba, kwa kuichapa Brighton bao 1-0, juzi Jumanne.

Kabla ya Sikukuu ya Krismasi, gwiji wa England na mchambuzi wa soka kwa sasa, Alan Shearer alikuwa miongoni mwa watu waliohoji kama 'Washikabunduki' hao wataweza kubakia kwenye Ligi Kuu msimu huu.

Kichapo kutoka kwa Everton, Desemba 19, kiliwaacha wakiwa pointi nne juu kutoka mstari wa kushuka daraja baada ya kucheza mechi 14 ukiwa ni mwanzo wao mbaya zaidi tangu msimu wa 1974-75.

Lakini mambo yakabadilika kwa ushindi wa kushangaza wa 3-1 dhidi ya Chelsea wikendi iliyopita, ambapo sasa wamefuatiwa na ushindi mwingine juzi.

"Kwa wakati huu, tunajua namna gani tunahitaji ushindi," alisema Arteta akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo wa ugenini.

"Kwa uhakika kabisa tulikuwa kwenye wiki ngumu na halikuwa tatizo tu la kiwango cha timu, ilikuwa ni matokeo mabaya ya timu.

"Unahitaji matokeo ili kuanza kujiamini na sasa tumepata ushindi mara mbili, nafikiri kila mmoja yupo kwenye hali nzuri."

Kwenye mchezo huo, Arsenal ilipata nafasi nyingi za kufunga wakati Pierre-Emerick Aubameyang na Gabriel Martinelli walipokosa nafasi za wazi za kufunga, kabla ya Alexandre Lacazette kufunga bao pekee na la ushindi katika dakika ya 66.

Arsenal imejivuta hadi nafasi ya 13 ikiwa na pointi 20, huku Brighton ikibaki ikiwa juu kwa pointi mbili kutoka mstari wa kushuka daraja, katika nafasi ya 17.

# MILIK KUMRITHI COSTA ATLETICO

**MADRID, Hispania**

KLABU ya Atletico Madrid ipo kwenye mkakati mpana wa kumsajili mshambuliaji nyota wa Napoli, Arkadiusz Milik ili kuwa mbadala wa Diego Costa.



Costa ameomba kusitishwa kwa mkataba wake wakati wa dirisha dogo la Januari kwa makubaliano ya pande zote ili aweze kurejea Amerika ya Kusini kwa sababu zake binafsi.

Milik anazidi kuonekana kama chaguo la kwanza kama mbadala wake, na kwa mujibu wa vyanzo vya AS, Mundo Deportivo na Marca, vyote vinamtaja mchezaji huyo wa kimataifa wa Poland kuingia kwenye malengo ya Atletico.

Milik hajapata fursa ya kuichezea Napoli msimu huu, baada ya kuachwa kikosini tangu alipokataa kusaini mkataba mpya au kukamilisha uhamisho wa kuhamia kwenda AS Roma.

Mkataba wake wa sasa na Napoli unamalizika Juni 2021 na hiyo inatajwa kuwa inaweza kuwa changamoto katika kukamilisha uhamisho wake kwenda Atletico, kwa kuwa anaweza kulazimika kusubiri miezi sita zaidi ili aweze kuwa mchezaji huru na kusajiliwa bure msimu ujao.

Napoli wanahitaji angalau euro milioni 15 kuachana na mshambuliaji huyo, pungufu ya dau la awali la euro milioni 18 walilokuwa wanaihitaji wakati wa kipindi cha msimu wa joto.



# JORDAN

## AWASHIWA TAA YA KIJANI ARSENAL

**LONDON, England**

MABOSI wa Klabu ya Arsenal wanahitaji saini ya nyota wa Sevilla, Joan Jordan ili kuongeza nguvu ndani ya kikosi hicho, kwa mujibu wa gazeti la Daily Mail.

Jicho la Kocha Mkuu wa Arsenal, Mikel Arteta, linatajwa kuitazama kwa ukaribu saini ya nyota huyo mwenye umri wa miaka 26 raia wa Hispania.

Ushindi wao wa mabao 3-1 dhidi ya Chelsea walioupata Desemba 26, mwaka huu umemfanya Arteta afikirie kuongeza nguvu eneo la kiungo ili kupata ushindi zaidi kwenye mechi zake.

Arteta ana matumaini kwamba akipata saini ya nyota huyo ataongeza nguvu ya kujiamini kwa kikosi chake kwa kuwa ana uwezo pia wa kufunga kwa kuwa ndani ya LaLiga akiwa amecheza jumla ya mechi 41 amefunga mabao mawili.

Arsenal ipo tayari kuweka dau la pauni milioni 32 ili kumpata nyota huyo ambaye amewahi kucheza pia ndani ya Klabu ya Eibar msimu wa 2017-19 na alicheza jumla ya mechi 71 na kufunga mabao 10.


## COSTA AVUNJA MKATABA WAKE NA ATLETICO MADRID

**MADRID, Hispania**

KLABU ya Atletico Madrid imetangaza kwamba, imefikia makubaliano ya pamoja na Diego Costa kusitisha mkataba wa mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Hispania.

Straika huyo wa zamani wa Chelsea, Costa aliwataka Atletico Madrid kumaliza mkataba mapema kutokana na sababu binafsi.

Mkataba wa mshambuliaji huyo na miamba hiyo ya LaLiga ulipangwa kumalizika Juni 2021, lakini ameiomba klabu hiyo kumalizana nao kwa sababu binafsi.



Taarifa ya Atletico ilisomeka: "Atlético de Madrid na Diego Costa wamefikia makubaliano ya kukatisha mkataba, ambao ungekamilika Juni 30, 2021.

"Mshambuliaji huyo aliomba kuondoka klabuni hapa kwa sababu binafsi siku chache zilizopita na Jumanne alisaini kusitishwa kwa mkataba wake.

"Klabu inamshukuru Diego Costa kwa kujitolea kwake katika miaka hii na inamtakia kila la heri katika hatua inayofuata."



## JUVE, REYNOLDS WAMALIZANA

**TURINI, Italia**

JUVENTUS imefikia makubaliano na wamekubaliana na Klabu ya FC Dallas kwa ajili ya kumsajili nyota wake, Bryan Reynolds, ambaye anatarajiwa kupelekwa kwa mkopo Cagliari.

Kwa mujibu wa ripoti kutoka nchini Italia, Juventus imekubali kulipa dau la dola milioni 10 kwa ajili ya kupata saini ya mchezaji huyo.

Staa huyo anayecheza nafasi ya ulinzi, alikuwa pia anahusishwa na Klabu za AS Roma, Club Brugge na Juventus ndio walioweza kuinyaka saini yake.

Reynolds alisaini mkataba mpya na FC Dallas Septemba mwaka huu ambao ungefika tamati mwaka 2024.

Kinda huyu mwenye umri wa miaka 19, ametokea kwenye akademi ya FC Dallas, na kwa mujibu wa ESPN makubaliano yamefanyika kwa dau la dola milioni 10, na Juventus watampeleka nyota huyu chipukizi kutumikia kwa mkopo ili kupata uzoefu.

Ripoti zinataja kuwa kwa mujibu wa makubaliano, Cagriali watamchukua nyota huyu kwa mkopo wa miezi sita.

Hii inakamilisha idadi inayotarajiwa ya wachezaji wa nje ya Ulaya ambao Juventus wanahitaji kuwa nao kwa msimu huu.

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# RASHFORD: TUSIFIKIRIE UBINGWA MAN UNITED

●●●Ni upuuzi, tunatakiwa kuangalia kila mchezo mbele yetu na kama tunaweza kutafuta njia…

**MANCHESTER, England**

MARCUS Rashford amesisitiza kwamba ni "upuuzi" kwa Manchester United kuanza kufikiria ubingwa wa Ligi Kuu England, baada ya kupunguza wigo wa pointi hadi mbili dhidi ya vinara Liverpool, na sasa wakiwa nafasi ya pili.

Rashford alifunga bao dakika za nyongeza kuiwezesha Man United kuibuka na ushindi wa 1-0 dhidi ya Wolves, juzi Jumanne usiku.

Nyota huyo wa England alifunga bao hilo akiunganisha pasi ya mwisho kutoka kwa Bruno Fernandes kwenye mchezo huo uliopigwa pale kwenye dimba la Old Trafford.

Hata hivyo, baada ya mchezo huo, Rashford alikataa kuzungumzia nafasi ya ubingwa kwa kikosi hicho na kusema utakuwa ni "upuuzi" kuangalia msimamo wa ligi wakati zikiwa zimechezwa mechi 15 pekee.

"Nafikiri kwa sisi hatuwezi kuangalia mbele zaidi kuhusu ubingwa kwa sasa," alisema Rashford akiiambia Amazon Prime.

"Sisi ni timu ambayo bado tunafanya kazi nyingi na haiwezekani kwa sasa kuangalia msimamo wa ligi, kwani ni mapema mno na utakuwa upuuzi kwa upande wetu.

"Tunatakiwa kuangalia mchezo kila mchezo mbele yetu na kama tunaweza kutafuta njia ya kushinda zaidi mwisho wa msimu ndio tutaona tupo sehemu gani." Bao hilo la Rashford lilikuwa la saba katika mechi 15 za Ligi Kuu msimu huu, baada ya kufunga mara 17 katika mechi 31 msimu wa 2019-20.

Naye kocha wa Man United, Ole Gunnar Solskjaer alibainisha kwamba aliwapa hamasa kubwa wachezaji wake na kuwataka kufikiria mechi zinazofuata na si ushindi walioupata.

"Kwa sasa tunaangalia mechi za mbele, hatutakiwi kufikiria sana kuhusu ushindi wa leo (juzi), maana bado kuna safari ndefu sana kwenye ligi," alisema Solskjaer.

## KWA UFUPI

**ARSENAL YAMTAKA ISCO**

ARSENAL wanawania kumsajili mshambuliaji wa Real Madrid, Isco mwenye umri wa miaka 28, wakati dirisha la uhamisho Januari. 'Washikabunduki' hao wanataka kumsajili mchezaji huyo kwa mkopo, lakini wanakabiliwa na ushindani kutoka kwa Sevilla. ***(AS, via Metro)***

**WIDJNALDUM KUAMUA**

KIUNGO wa kati wa Uholanzi, Georginio Wijnaldum mwenye umri wa miaka 30, ataamua wiki hii iwapo atatia saini mkataba mpya na Liverpool, huku kocha wa Barcelona, Ronald Koeman akiwa na matumaini ya kumshawishi kiungo huyo kujiunga naye. Mkataba wa sasa wa Wijnaldum, ambaye amekuwa Anfield tangu 2016 unakamilika Juni mwakani. ***(Sky Sports)***

**MAN CITY BADO KWA MESSI**

MANCHESTER City bado ina matumaini ya kumsajili mshambuliaji wa Barcelona, Lionel Messi mwenye umri wa miaka 33, mwaka 2021, licha ya nahodha huyo wa Barca kusema kwamba, anatumaini siku moja atacheza soka nchini Marekani. ***(Telegraph)***

**ARSENAL YAMTOSA AOUAR**

ARSENAL haitaendelea na mpango wake wa kutaka kumsajili nyota wa Lyon na Ufaransa, Houssem Aouar wakati wa dirisha dogo la usajili la Januari. ***(The Athletic)***

**LIVER YAACHANA NA SKRINIAR**

LIVERPOOL imeachana na nia yake ya kutaka kumsajili mlinzi wa Inter Milan, Milan Skriniar mwenye umri wa miaka 25, baada ya kukasirishwa na dau la pauni milioni 54 lililowasilishwa na klabu hiyo ya Italia. ***(Calciomercato)***

**ALONSO KURUDI ATLETICO**

MLINZI wa Chelsea na Hispania, Marcos Alonso, mwenye umri wa miaka 30, anatarajiwa kurudi nyumbani kwao kujiunga na Atletico Madrid kwa mkopo katika dirisha la Januari. Alonso hajaichezea Chelsea tangu Septemba 26, mwaka huu. ***(Independent)***

**CAPELLO AMKUBALI DYBALA**

KOCHA wa zamani wa timu ya Taifa ya England na klabu ya Juventus, Fabio Capello, amesema yeye angemchagua Paulo Dybala mwenye umri wa miaka 27 badala ya straika wa England, Harry Kane mwenye umri wa miaka 27. ***(Gazzetta dello Sport)***

**POCHETTINO KUIBOMOA SPURS**

MAURICIO Pochettino anatarajiwa kuwasajili baadhi ya wachezaji wa Tottenham Hotspur akiwamo kiungo mshambuliaji, Dele Alli mwenye umri wa miaka 24, na kipa wa Ufaransa, Hugo Lloris, iwapo raia huyo wa Argentina atathibitishwa kuwa kocha mpya wa Paris-St Germain. ***(Eurosport)***

**WOLVES WAMTAKA COSTA**

KLABU ya Wolves huenda ikawasilisha ombi la kumsajili, Diego Costa mwenye umri wa miaka 32, kuchukua nafasi ya mshambuliaji, Raul Jimenez mwenye miaka 29, baada ya straika huyo wa Hispania kusitisha mkataba na Atletico Madrid na kuwa mchezaji huru Januari. ***(Times)***

**SPURS YAMWINDA SABITZER**

TOTTENHAM Hotspur ina nia ya kumsajili kiungo wa kati wa Austria, Marcel Sabitzer, mwenye umri wa miaka 26, wakati wa dirisha dogo la Januari, kwa mujibu wa klabu yake RB Leipzig. ***(Evening Standard)***

HABARI MICHEZO

# POLISI TANZANIA, AZAM MCHUANO WA HESHIMA

**Na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati, amesema timu yake itacheza kwa kiwango cha juu katika mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya wenyeji Polisi Tanzania kwenye Uwanja wa Ushirika Mjini Moshi, ili kupata pointi tatu na kurejesha heshima yake kwenye ligi hiyo.

Kikosi cha Azam FC kiliwasili salama Moshi jana asubuhi tayari kwa kuanza kusaka pointi tatu muhimu kwenye mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana asubuhi kabla ya kuanza safari, Bahati alisema wamejiandaa vizuri kwenda kukabiliana na Polisi Tanzania na wanaamini watarejea na ushindi.

Bahati alisema wenyeji wao, Polisi Tanzania wana kikosi kizuri na chenye wachezaji wazuri, hivyo wamejiandaa kukutana na mchezo mgumu.

"Tumesafiri na wachezaji 19, akiwamo Salum Aboubakary (Sure Boy) ambaye alikuwa majeruhi, amerejea kikosini, tunafahamu mechi ngumu ila tumejipanga kutafuta pointi tatu muhimu.

"Kuhusu mchezaji, Mpiana Monzinzi, hayumo kwenye kikosi kinachosafiri kuelekea Moshi, mambo yake hayajakuwa sawa ikiwamo vibali," alisema kocha huyo.

Aliwataka wachezaji ambao bado ni majeruhi, lakini wameshaanza mazoezi mepesi kuwa ni pamoja na Abdallah Kheri (Sebo) na Prince Dube. Naye Kocha Mkuu wa Polisi Tanzania, Malale Hamsini, alisema kikosi chake kipo fiti na kitahakikisha kinapambana kubakiza pointi tatu nyumbani.

Alisema itakuwa mechi ya kisasi kwa sababu ile ya duru la kwanza walipoteza wakiwa ugenini kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi.

"Ni mechi ya ushindani mkubwa kwa sababu tumejipanga kutumia vema uwanja wa nyumbani, lakini wenzetu nao wanahitaji matokeo mazuri kulingana na mahitaji yao pia ukizingatia wenzetu hawakuwa na matokeo mazuri mechi zao za mwisho," alisema Malale.

Mechi nyingine za ligi hiyo zitakazochezwa leo ni kati ya Tanzania Prisons dhidi ya vinara Yanga, huku Coastal Union wakiwakaribisha Namungo FC kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini, Tanga.

IKO HIVI...



Rais wa Shirikisho la Riadha Tanzania (RT), Anthony Mtaka, akiongoza kikao cha mkutano mkuu wa shirikisho hilo, kilichofanyika jijini Dar es Salaam jana, kujadili mabadiliko ya katiba. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Hitimana asikitika kumkosa Ilanfya

**Na Saada Akida**

BAADA ya kushindwa kufanya usajili kipindi cha dirisha dogo, Kocha Mkuu wa Mtibwa Sugar, Thiery Hitimana, amesema ana kazi ya ziada kuhakikisha kikosi cha timu hiyo kinafanya vizuri kwenye mechi za lala salama ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Moja ya mapendekezo ya kuboresha kikosi hicho, Hitimana alimhitaji mshambuliaji mmoja huku akimpendekeza nyota wa Simba, Charles Ilanfya, lakini juhudi za kumpata straika huyo zilishindikana.

Akizungumza na gazeti hili jana, Hitimana alisema kutokana na hali hiyo, amejiandaa kuhakikisha wanafanya vizuri kwa kutumia wachezaji aliowakuta kwa kuwapa mbinu mbalimbali zitakazowavusha kwenye janga la kutoshuka daraja.

Hitimana alisema kwa sasa kila mchezaji anamkabidhi majukumu yake kulingana na nafasi yake, huku akitoa programu maalumu kwa washambuliaji wake ili waongeze umakini wanapopata nafasi za kufunga.

"Tunatakiwa kupambana, hasa ukizingatia timu tunazokwenda kupambana nazo zimejiimarisha kipindi hiki cha dirisha dogo, hapa kwetu hatujafanya usajili, kwa staili ya kutofanya maboresho kwenye kikosi, ni ngumu sana kumaliza katika nafasi tano za juu," alisema Hitimana.

Aliongeza hakuna mechi nyepesi, lakini anaamini wachezaji wake wakitekeleza maelekezo yake, watafikia malengo yaliyopo ya klabu hiyo kwa sasa.

Alisema kikosi cha timu yake kinaondoka leo Morogoro kuelekea jijini Dar es Salaam na baadaye kuifuata Ruvu Shooting katika mchezo wa Ligi Kuu Bara utakaochezwa Jumamosi ya Januari 2, mwakani kwenye Uwanja wa Mabatini, Pwani.

## Simba SC yatoa darasa Majimaji

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Majimaji, Peter Mhina, amesema kipigo cha mabao 5-0 walichokipata kutoka kwa mabingwa watetezi wa Kombe la FA, Simba, kimewaimarisha kuelekea mchezo wao wa Ligi Daraja la Kwanza dhidi ya Lipuli utakaochezwa keshokutwa, Ijumaa.

Mhina, beki wa zamani wa Majimaji, aliliambia gazeti hili mechi hiyo ya Kombe la FA imewapa wachezaji wake mbinu mpya, hivyo anaamini wanauwezo wa kuifunga Lipuli na kujiweka kwenye nafasi nzuri katika msimamo wa Kundi A wa Ligi Daraja la Kwanza.

"Tumepoteza mechi dhidi ya timu kubwa, timu bora Tanzania, hatuangalii kwa nini tumefungwa na Simba, ila tunaangalia jinsi tulivyocheza na kitu gani tumejifunza kwa ajili ya mechi zetu zinazokuja, ukianzia na mechi hii dhidi ya Lipuli," alisema Mhina.

Jumapili iliyopita, Majimaji ilitolewa katika mashindano ya Kombe la FA baada ya kukubali kichapo kutoka kwa 'Wekundu wa Msimbazi' kwenye mechi ya raundi ya tatu iliyochezwa katika Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Ofisa Habari wa Lipuli, Clement Sanga, alisema timu yake imejiandaa kuwazidishia machungu ya kufungwa na Simba kwenye mechi hiyo ya Ligi Daraja la Kwanza.

"Najua bado wamechanganyikiwa na kipigo cha Simba, na sisi kabla hawajakaa sawa tutapiga hapo hapo," alisema Sanga ambaye timu yake imejipanga kurejea kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

## Namungo yapiga mahesabu Afrika

**Na Shufaa Lyimo**

NAHODHA wa Namungo FC, Hamisi Fakhi, amesema timu yao iko imara na haina hofu yoyote kuelekea mchezo wao wa marudiano wa mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya El Hilal Obeid utakaochezwa Januari 5, mwakani jijini Khartoum nchini Sudan.

Katika mechi ya kwanza iliyochezwa wiki iliyopita kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam Namungo ilishinda mabao 2-0.

Fakhi aliliambia gazeti hili kuwa, kupitia mchezo wa kwanza wamefanikiwa kuwasoma vizuri wapinzani wao, hivyo hawawezi kusumbuka katika mchezo huo wa marudiano.

Nyota huyo alisema siri nyingine inayowafanya wafanye vizuri kwenye mashindano hayo ni umoja waliokuwa nao wachezaji kwa ajili ya kufikia malengo ya pamoja.

"Tayari tumeshajua udhaifu wa wapinzani wetu, hata tukienda kwao tunafahamu sehemu ya kuwabana ili wasiweze kupata nafasi ya kutufunga," alisema nahodha huyo.

Hata hivyo, nyota huyo amewaomba Watanzania kuzidi kuwaamini kwa sababu watakwenda Sudan kwa lengo la kuiwakilisha vema nchi.

Michezo

Alhamisi Desemba 31, 2020

Nipashe



RASHFORD: TUSIFIKIRIE UBINGWA MAN UNITED

HABARI UK 22

'HOME IMEJIBU'...!



Kiungo Clatous Chama na mshambuliaji Meddie Kagere (katikati), wakishangilia pamoja na mfungaji wa bao la kwanza, Mohamed Hussein 'Tshabalala' (kulia), wakati Simba ikiibuka na ushindi wa mabao 4-0 kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Ihefu FC iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa jana. Wachezaji kuweka mpira tumboni wanapofunga huashiria ndoa nyumbani imejibu. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# SIMBA YAFUNGA MWAKA KWA 4G

●●●Kagere, Mugalu kama kawa kambani, Manula asema sasa bado FC Platinum...

**Na Adam Fungamwango**

MABAO matatu yaliyofungwa na mastraika wa Simba Meddie Kagere na Chriss Mugalu na moja la beki wa kulia Mohamed Hussein 'Zimbwe Jr', yameifanya timu hiyo jana kufunga mwaka huu kwa kuondoka na ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Ihefu FC katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, kwenye mechi ya kwanza ya mzunguko wa pili Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mechi hiyo ni ya mwisho kwa Simba mwaka huu wa 2020, kwani haitashuka tena dimbani hadi Jumatano ijayo, Januari 6, mwakani itakapoikaribisha FC Platinum ya Zimbabwe katika uwanja huo kwenye mchezo wa marudiano wa Ligi ya Mabingwa Afrika kuwania kufuzu hatua ya makundi.

Aidha, ushindi huo kwa Simba ni mwendelezo mzuri kwao kuifunga Ihefu FC, baada ya mechi ya mzunguko wa kwanza iliyochezwa Septemba 6, mwaka huu kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya, kushinda kwa mabao 2-1.

Lakini kwa mabao hayo, Mnyarwanda Kagere alijiongezea mawili na kufikisha mabao saba kwenye orodha ya wafungaji, huku Mkongomani Mugalu akifunga bao na kufikisha jumla ya mabao manne kibindoni.

Simba ilianza biashara asubuhi tu dakika ya tisa, ilipopata bao la kwanza, likifungwa na Zimbwe Jr baada ya kupokea pasi ya pembeni kutoka kwa beki mwenzake wa pembeni, Shomari Kapombe, likiwa ni bao lake ya kwanza msimu huu kwenye Ligi Kuu.

Kuingia kwa bao hilo kulionekana kuwachangamsha wachezaji wa Simba na kufanya mashambulizi mfululizo, wakikosa mabao mengi ya wazi, hadi ilipofika dakika ya 15, straika hatari wa timu hiyo, Kagere alipofunga kwa shuti kali la mbali baada ya kupokea pasi kutoka kwa Luis Miquissone, na kuachia shuti kali lililomshinda Deogratius Munishi 'Dida'.

Kagere kwa mara nyingine tena alifunga bao rahisi akiwa yeye na wavu dakika ya 40, kutokana na kazi nzuri ya Clatous Chama aliyewatoka mabeki wa Ihefu.

Shambulizi pekee la hatari kwa Ihefu lilikuwa dakika ya 45, wakati mchezaji aliyesajiliwa kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili, Joseph Mahundi, alipokokota mpira kuanzia katikati ya uwanja bila kukabwa na wachezaji wa Simba, akaachia shuti kali lililopita juu kidogo la lango la Simba, akiacha kipa Aishi Manula akiwalalamika viungo wake.

Kipindi cha pili Ihefu ilionekana kubadilika na kukamata eneo la kiungo, hivyo kuipa shida Simba kwa muda mrefu. Ni kipindi ambacho Simba ilionekana kufanya mashambulizi kwa kushtukiza na ilipofika dakika saba kabla ya pambano kumalizika, Mugalu alipata pasi safi kutoka kwa Chama.

Kwa matokeo hayo, Simba bado inaendelea kuwa kwenye nafasi ya pili na pointi 35, hivyo kupunguza idadi ya pointi kwa vinara Yanga ambao wamejikusanyia pointi 43 mpaka sasa.

Baada ya mechi hiyo, Kipa wa Simba, Manula alisema, ushindi huo ni chachu kubwa ya kufanya vizuri kwenye mechi ijayo dhidi ya FC Platinum.

"Siunajua Simba ikiwa nyumbani kwenye mechi za kimataifa, kufungwa bao moja ugenini kwetu si tatizo, tutaingia tukijua nini tunakitafuta kama wawakilishi wa nchi," alisema Manula.

## YANGA, PRISONS VITA VYA KIBABE

**Na Somoe Ng'itu**

VINARA wa Ligi Kuu Bara, Yanga, wanatarajia kuendelea na kampeni ya kuwania taji la ligi hiyo watakapokutana na wenyeji, Tanzania Prisons, leo kwenye Uwanja wa Nelson Mandela mjini Sumbawanga mkoani Rukwa.

Kikosi cha Yanga kiliwasili Sumbawanga jana mchana na kupata mapokezi makubwa kutoka kwa wanachama na mashabiki wa timu hiyo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Yanga, Cedric Kaze, alisema kikosi chake kiko vizuri na kimejiandaa vema kuhakikisha kinaendelea kupata matokeo chanya kwenye ligi hiyo.

Kaze alisema wataingia dimbani wakiwa makini zaidi kwa sababu Prisons ni moja ya timu zenye matokeo mazuri na yenye wachezaji waliokaa pamoja kwa muda mrefu.

"Tumefika salama, kikosi kiko vizuri na tuko tayari kwa mchezo wetu dhidi ya Prisons, ninaamini tutafanya kile tulichokipanga, ila haitakuwa mechi rahisi, wenyeji wetu pia wamejiandaa kupata matokeo," alisema Kaze.

Aliwataja wachezaji watatu ambao wako katika hatihati ya kuwatumia kutokana na kuwa majeruhi na hawatakuwa sehemu ya mechi ya leo ambao ni pamoja na golikipa Ramadhani Kabwili, Saido Ntibazonkiza na Yacouba Songne.

"Tumejipanga kulingana na uzito wa mechi, kila mechi huandaliwa tofauti, itakuwa ni mechi ngumu sana, tunapaswa kucheza kwa kiwango cha juu, kila mechi ni dakika 90, tusubiri tuone," Kaze aliongeza.

Naye Kocha Msaidizi wa Tanzania Prisons, Shabani Kazumba, alisema watakutana na Yanga wakiwa na kumbukumbu ya kutoka nao sare ya bao1-1, walipokutana kwenye mzunguko wa kwanza.

"Tumejipanga vizuri, malengo yetu ni kupata ushindi ingawa tunajua haitakuwa mechi nyepesi, tunawaomba mashabiki wajitokeze kwa wingi uwanjani, tunasema hatutakubali kufungwa kirahisi," alisema kocha huyo.

Yanga yenye pointi 43 inakutana na Prisons yenye pointi 21 na iko kwenye nafasi ya 11 katika msimamo wa ligi hiyo ikishinda mechi tano, sare sita na imepoteza michezo sita.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002